**Wateja** watelekeza mabilioni ya fedha benki zilizofilisiwa

UKURASA 3



**Wanafunzi** walia na mapunjo fedha za mikopo elimu ya juu

UKURASA 3


# Nipashe

Ijumaa Februari 26, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580503

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Guardiola atambia fedha za Man City**

UKURASA 20



# Hatima ya kigogo IPTL sasa siku 30

• **Ni** kuhusu mazungumzo kumalizana na DPP... *Endelea Uk.2*



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile (wa pili kushoto), akionyesha SimBanking mpya ya Benki ya CRDB inavyoonekana, baada ya kujiunga wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela na (wa pili kulia) ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Benki hiyo, Prof. Neema Mori na Naibu Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Khadija Said. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Halima Mdee aachiwa huru kesi madai ya kukashfu Rais

UKURASA 3



## Magufuli awaonya wafanyabiashara kutumia machinga kukwepa kodi

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YAITISHA AFRICAN LYON** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM awaonya wafanyabiashara kutumia machinga kukwepa kodi

**Na Romana Mallya**

RAIS John Magufuli amewaonya wafanyabiashara wakubwa wanavyokwepa kodi ya serikali kwa kuwatumia machinga kuuza bidhaa zao.

Alitoa onyo hilo jana, alipohutubia wananchi baada ya kuzindua jengo la Jitegemee lililoko Lumumba jijini Dar es Salaam ambalo ndani yake, zimo ofisi za vyombo vya habari vinavyomilikiwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Vilevile, Rais Magufuli aliweka jiwe la msingi katika Soko la Kisutu ambalo litakapokamilika litakuwa na uwezo wa kuhudumia wafanyabiashara 1,500 wakati awali lilihudumia 669.

Akizungumza katika viwanja vya Mnazimmoja, Rais Magufuli alisema katika suala la kodi, wapo baadhi ya wafanyabiashara ambao siyo waaminifu, wanawatumia machinga kufanya biashara zao ili kukwepa kodi.

"Mfanyabiashara anakuwa na stoo halafu anapeleka biashara kule. Unakuta anayefanya biashara kweli siyo machinga, bali ni mfanyabiashara mkubwa na mali ni za mfanyabiashara, siyo machinga.

"Ninatoa wito kwa TRA (Mamlaka ya Mapato) ambao wakati mwingine wamekuwa wakitoa makadirio makubwa sana kwa wafanyabiashara na wafanyabiashara wanaacha au wanatafuta mbinu nyingine ya kukwepa kodi, mfuatilie," aliagiza.

Rais Magufuli aliitaka TRA ijifunze katika kutoa haki kwa wafanyabiashara ambao wana nia nzuri ya kulipa kodi.

"Ninaamini yote yakienda kwa pamoja, tutafanikiwa kwa sababu saa nyingine TRA nako kuna wafanyakazi ambao ni wala rushwa. Anakwenda anakukadiria cha juu sana ili ukishindwa kile utakachokuwa nacho ugawane naye.

"Lazima TRA wajirekebishe, nitoe wito kwa Wizara ya Fedha na Mipango, mkasimamie haya kwa sababu tunahitaji kodi, tunahitaji ushuru, lakini uwe wa haki kwa watu wanaolipa," aliagiza.

Vilevile, alisema amepokea malalamiko ya wafanyabiashara kuhusu gharama za uzoaji taka ambazo ni kati ya Sh. 20,000 hadi 250,000.

"Maduka ya vifaa vya ujenzi hutozwa Sh. 50,000, maduka ya dawa hutozwa Sh. 200,000. Ninajua jiji limepatikana, malalamiko mengine yatafanyiwa kazi ili kurekebisha," alisema.Rais Magufuli alisema lipo tatizo la wafanyabiashara kuacha kutoa risiti na kuweka bei tofauti kwa bidhaa zinazokatiwa risiti na zisizokatiwa risiti na kuviagiza vyombo husika visimamie suala hilo.

"Wafanyabiashara kuweni waaminifu unapotoa risiti ndogo wakati mtu kalipa kingi, ni wizi! Fedha zinazohitajika ndizo zinatumika kwa ajili ya maendeleo," alisisitiza.

Alimtaka Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Suleiman Jafo, kuhakikisha vitambulisho vya wajasiriamali wadogo vinatolewa.

Kuhusu Soko la Kisutu na mengine yanayojengwa, Rais Magufuli alisema yanawawezesha wakulima wauze bidhaa zao kwa bei nzuri.

Alisema masoko hayo pia yanaiwezesha serikali kufahamu matatizo ya wafanyabiashara kwa kufanya tathmini ya uzalishaji na matumizi kwa walaji.

"Mpaka sasa masoko yaliyojengwa ni 24, yapo yaliyokamilika na mengine bado, yanajengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 119.9. Tumejenga pia stendi karibu 18, haya yote ni katika kuboresha miji yetu.

"Soko la Kisutu ni miongoni mwa miradi saba inayotekelezwa Dar es Salaam, masoko mengine ni Magomeni, Tandale, Kibada, Mburahati, Machinjio Vingunguti na Kituo Kikuu cha Mabasi Mbezi Luis," alisema.

Alisema Soko la Kisutu litakapokamilika litakuwa na vizimba zaidi ya 500 na machinjio ya nyama, kuku, migahawa, mama lishe na baba lishe, huduma za kibenki na maegesho ya magari 43 kwa wakati mmoja na ofisi za huduma nyingine.




Rais Dk. John Magufuli akifungua jiwe la msingi la jengo jipya la Soko Kuu la Kisutu, katika Barabara ya Bibi Titi Mohamed, jijini Dar es Salaam jana. Watatu kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Selemani Jafo na (wapili kushoto) ni Mbunge wa Ilala, Mussa Azzan Zungu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Siku 30 sasa kuamua hatima kigogo IPTL

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imetoa siku 30 kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) na mmiliki wa Kampuni ya Kufua Umeme ya Independent Power Tanzania Limited (IPTL), Habinder Seth pamoja na Mwanasheria wa kampuni hiyo, Joseph Mwakandege, kukamilisha mchakato wa makubaliano ya kumaliza kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili.

Hata hivyo, Mahakama hiyo imesema DPP ana mamlaka ya kukubali au kukataa maombi yanayowasilishwa kwake ikiwamo kuingia kwenye makubaliano ya kumaliza kesi na washtakiwa, na kwamba halazimishwi kufanya hivyo kisheria.

Amri hiyo ilitolewa jana katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Awali, wakili wa utetezi, Melchisedeck Lutema na Mwakandege waliwasilisha malalamiko yao kuwa wateja wao wamemwandikia DPP barua ya kuomba kufanya makubaliano zaidi ya mara mbili, lakini hawajapata majibu.

Wakili Lutema alidai kuwa mteja wake alimwandikia DPP barua Julai Mosi, 2019 na ilipokolewa ofisini kwake Julai 23, 2019, barua ya pili Seth aliiandika Julai 20, 2020 na kupokelewa Septemba 10, 2020 bila majibu.

Aidha, alidai utetezi unaifahamisha mahakama kuwa mteja wake yuko tayari kuingia makubaliano na DPP ya kumaliza kesi na pia kwa mujibu wa Kanuni ya 3 ya makubaliano mapya zilizotolewa na Jaji Mkuu mwaka 2021, chini ya Kifungu cha 5 cha kanuni hizo, mahakama ina mamlaka ya kutoa muda kwa pande husika kujadiliana na kukamilisha makubaliano ya kumaliza kesi kwa muda wa siku 30.

"Mheshimiwa hakimu, tunaomba siku 30 ili tuendelee na mchakato na DPP," Lutema aliiambia mahakama.

Aliendelea kudai kuwa Juni 2, 2021 Sethi aliiandikia mahakama hiyo barua ya malalamiko na kupokelewa Februari Mosi, 2021, kuwa hakuletwa mahakamani ndani ya miezi saba.

Alidai kuwa hayo yote yamekuwa yakifanyika bila sababu yoyote, licha ya kuwa ni takwa la kisheria mahabusu kuletwa mahakamani ndani ya siku 14, kwa hiyo anaomba safari ijayo mteja wake aletwe mahakamani.

Kwa upande wake, Sungwa aliieleza Mahakama kuwa mteja wake (Mwakandege) aliandika barua Januari 8, 2021, kwa DPP akiomba makubaliano ya kumaliza kesi, hivyo kuiomba Mahakama itoe maelezo.

Akijibu homa hizo, Wakili wa Serikali, Faraja Ngukah, alidai katika suala la kutokuletwa mahakamani katika kumbukumbu zake mara ya mwisho kuletwa mahakamani ilikuwa Desemba 17, 2020 kwa hiyo si kweli kuwa miezi saba hawakuletwa mahakamani.

"Ni kweli sheria inataka ndani ya siku 14 washtakiwa waletwe mahakamani na pale ambapo tumeshindwa kuwaleta tunatoa sababu na kuonyesha kwamba kuwa hatuma nia mbaya... wamekuwa wakiomba ahadi ya kuwaleta mahakamani, kwa hiyo hakuna haja ya mahakama kutoa amri hiyo tena," alidai Ngukah.

Kuhusu suala la makubaliano, Ngukah alidai kwa sababu mahakama imeshapewa taarifa, utaratibu ufuatwe uliyoelekezwa kisheria, lakini yeye hana barua ambazo walizizungumzia.

"DPP ana mamlaka kisheria ya kuingia makubaliano au la, hawezi kulazimishwa kuingia kwenye makubaliano," alidai.

Baada ya kusikiliza hoja hizo, Hakimu Shaidi alisema kuhusu suala la washtakiwa kutokuletwa mahakamani, sheria iko wazi hivyo ifuatwe, ndani ya siku 14 waletwe mahakamani.

"DPP ana mamlaka ya kukubali au kukataa kuingia kwenye makubaliano na halazimishwi, lakini sio kukaa kimya kwa kuwa Jaji Mkuu ameshatoa kanuni mpya, ambazo zinaelekeza mahakama kutoa maelekezo.

"Basi hilo lifanyike ndani ya siku 30 kuanzia leo (jana), na kesi itakuja tena kwa kutajwa Machi 11, 2021," alisema Hakimu Shaidi.

Mbali na Seth na Mwakandege, mshtakiwa mwingine ni mfanyabiashara, James Rugemalira, ambao wanakabiliwa na mashtaka 12.

Miongoni mwa mashtaka hayo yapo ya kula njama, kujihusisha mtandao wa uhalifu, kughushi na kutoa nyaraka za kughushi na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kutakatisha fedha na kusababisha hasara ya Dola za Marekani 22,198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.

Washtakiwa wanadaiwa kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi 19, 2014 jijini Dar es Salaam walikula njama katika nchi za Afrika Kusini, Kenya na India ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Makandege, anakabiliwa na mashtaka matano likiwamo la kuisababishia serikali hasara ya Dola za Marekani 980,000.

# Wanufaika HESLB walia kupewa fedha pungufu

**Maulid Mmbaga na Joseph Bartazaly**

BAADHI ya wanafunzi wa Chuo cha Uhasibu (TIA) wamelalamika kupewa fedha pungufu na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) na kuwa hatarini kutoruhusiwa kufanya mitihani ya chuo kwa kushindwa kulipa ada yote.

Mmoja wa wanufaika hao aliiambia Nipashe Dar es Salaam jana kuwa wiki tatu zilizopita, walikamilisha taratibu zote za mikopo, lakini Jumatatu ya juma hili walipewa taarifa ya kupunguzwa kwa fedha za mkopo wa ada ya chuo pasi na kuambiwa kiini cha uamuzi huo.

Alisema kuwa baadhi ya wanafunzi walibaini kudaiwa fedha nyingi na chuo tofauti na walivyotarajia, yote yakiwa ni matokeo ya fedha za mkopo kupunguzwa.

Mwanafunzi huyo alisema jambo hilo limeleta mkanganyiko kwa kuwa huenda baadhi ya wanafunzi wakashindwa kufanya mitihani kwa kutokukamilisha ada kwa wakati, akibainisha kuwa uongozi wa chuo hauruhusu mwanafunzi kufanya mtihani ikiwa hajalipa ada walau kwa asilimia 70.

"Wiki tatu zijazo tunatarajia kuanza kufanya mitihani na hatutaruhusiwa kufanya kama hujakamilisha ada na tumejaribu kuwasiliana na watu wa vyuo vingine ili tujue kama kuna jambo la namna hii, wanasema hakuna.

"Tulipowasiliana Bodi ya Mikopo, walisema walishatoa taarifa kwa maofisa mikopo ndani ya vyuo, lakini maofisa hao hawakutoa taarifa kwetu sisi wanufaika wa mkopo," alilalamika.

Baada ya kupata taarifa hizo, Nipashe ilimtafuta Ofisa Habari Mwandamizi wa HESLB, Veneranda Malima, ambaye alikiri bodi hiyo kupata malalamiko hayo na kubainisha suala hilo limefanyika kwa vyuo vyote nchini.

Alisema kuna baadhi ya wanafunzi waliongezwa kiwango cha kupokea fedha ya ada tofauti na kile walichotia saini awali na mwaka huu bodi imerudisha kiwango halisi walichotakiwa kupokea, hivyo haijapunguza fedha kama wanavyodai.

"Kuna baadhi viwango vilionekana vimepanda na wengine vimeshuka, lakini kama bodi tuliona tuwarudishie vile viwango stahiki walivyotakiwa kupokea tangu mwanzo," alisema.

Alisema walishafanya mazungumzo na viongozi wa Serikali ya Wanafunzi wa TIA wanaohusika na mikopo ya mwanafunzi na kuwafafanulia kuhusu suala hilo.

Nipashe pia ilimtafuta Ofisa Mikopo wa TIA, Hasani Ayubu, ambaye katika ufafanuzi wake kuhusu suala hilo, alisema idadi ya wanafunzi wanaopatiwa mikopo imeongezeka katika orodha ya kulipiwa ada na serikali na ndicho kiini cha malalamiko hayo.

Wakati baadhi ya wanafunzi wakilalama kupunguzwa kwa fedha za mkopo wa ada, wapo wenzao walioongezwa kiwango cha mkopo huo baada ya awali kupewa fedha kidogo kwa ajili ya ada ya chuo.

Alisema baada ya ongezeko hilo, wale walioongezewa ada mwaka jana, mwaka huu wamepunguziwa na hapo ndipo tatizo lilipoanzia kutokana na wahusika kutoridhishwa na uamuzi huo.

"Jambo hilo limefanyika kwa vyuo vyote nchini, siyo TIA tu. Mwaka huu wale wote wanaosema wamepunguziwa ada, ni zile walizoongezewa mwaka jana.

"Bodi ya Mikopo ilitoa taarifa kwa maofisa wa kila chuo kuhusu suala hilo na tunachokifanya kama viongozi, ni kuwasaidia waweze kuruhusiwa kufanya mitihani kwa wale wasiokamilisha ada," alisema.



Wafanyakazi watano wa kampuni ya Beertech Company Ltd, wakiwa chini ya ulinzi wa askari Polisi baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam jana, na kusomewa mashtaka ya utakatishaji fedha zaidi ya sh. bilioni nne. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mdee aachiwa huru kesi madai ya kumkashifu Rais

**Na Hellen Mwango**

MBUNGE wa Viti Maalumu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Halima Mdee, ameachiwa huru baada ya Jamhuri kushindwa kuthibitisha tuhuma za kutoa lugha ya uchochezi dhidi ya Rais Dk. John Magufuli.

Mdee aliachiwa huru jana na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Hakimu alisema baada ya kupitia ushahidi wa upande wa Jamhuri, bila kuacha shaka umeshindwa kuthibitisha kesi kwa Mdee.

"Jamhuri wana jukumu la kuthibitisha kesi bila kuacha shaka dhidi ya mshtakiwa. Katika kesi hii, ushahidi umeshindwa kuonyesha kama mshtakiwa ana kesi ya kujibu dhidi ya tuhuma zinazomkabili, mahakama hii inamwachia huru," alisema hakimu.

Alisema ushahidi wa mashahidi watatu wote askari polisi upande wa Jamhuri, umeshindwa kuthibitisha kuwa Mdee alitoa maneno ya uchochezi, hivyo mahakama imemwona hana hatia. Hakimu Simba alisema shahidi wa kwanza katika ushahidi wake, alidai kuwa yeye ndiye aliyeandika maelezo ya onyo ya mshtakiwa na maelezo hayo yalikataliwa mahakamani hapo, kwa hiyo ushahidi wake hakuthibitisha kosa alilokuwa akituhumiwa nalo.

Alisema shahidi wa pili katika ushahidi wake, alidai kuwa yeye aliona kwenye mtandao wa kijamii wa 'YouTube' mshtakiwa akitoa maneno ya uchochezi, lakini alishindwa kuyathibitisha mahakamani.

Kwa upande wa shahidi watatu, ambaye ni Mkuu wa Kituo cha Polisi cha Urafiki, yeye aliambatana na askari mwingine (Inspekta Patrick) kwenda kumkamata Mdee.

Akichambua uamuzi, hakimu alisema shahidi huyo aliagizwa kwenda kumkamata Mdee nyumbani kwa wazazi wake Ubungo, Dar es Salaam, ambako alimkuta mama yake na kumweleza kuwa anataka kumkamata mshtakiwa.

"Ushahidi pekee wa Jamhuri ni huu katika kesi hii unaothibitisha kuwa Mdee alikamatwa na kufunguliwa mashtaka haya," alisema Hakimu Simba.

Katika utetezi wake, Mdee alidai kuwa anamfahamu Rais wa Tanzania ni John Pombe Joseph Magufuli na hajui kama kumtukana Rais au mtu yeyote ni kosa la jinai. Alidai Machi 13, 2017 alikuwa mwanachama wa CHADEMA na Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA) na kwamba siku hiyo hapakuwapo na mkutano wa chama katika ofisi za makao makuu. Mdee alidai kuwa hajui kama kulikuwa na mkutano na waandishi wa habari siku hiyo na hakuna mashahidi waliosema siku hiyo kulikuwa na mkutano huo.

Akihojiwa na wakili wa utetezi Edson Kilatu, Mdee alidai Kinondoni hakuna mahali panapoitwa Ufipani na kwamba Makao Makuu ya CHADEMA yako Mtaa wa Ufipa.

Mdee anadaiwa kuwa Julai 3, 2017 katika Makao Makuu ya Ofisi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), mtaa wa Ufipa Manispaa ya Kinondoni, alitenda kosa la kutoa lugha chafu.

Anadaiwa alitamka maneno machafu dhidi ya Rais John Magufuli kuwa "anaongea ovyo ovyo, anatakiwa afungwe breki" na kwamba kitendo hicho kingesababisha uvunjifu wa amani.

# Wateja watelekeza mabilioni benki zilizofilisiwa

**Na Salome Kitomari,** MTWARA

BODI ya Bima ya Amana imesema wateja 38,654 kati ya 63,704 wa zilizokuwa benki saba ambazo zimefungiwa, hawajajitokeza kuchukua fedha zao ambazo wanapaswa kulipwa kwa mujibu wa sheria.

Aidha, wateja 25,050 ambao ni sawa na asilimia 39, walijitokeza kuchukua fedha hizo na wateja hao ni wale waliokuwa na viwango vikubwa na kwamba kati ya Sh. bilioni 11 zimechukuliwa Sh. bilioni 7.3.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana, Richard Malisa, wakati akiwasilisha mada ya bodi hiyo, mafanikio na changamoto.

Alizitaja Benki hizo kuwa ni Covenant Bank for Women (T) Limited, Efatha Bank Limited, Kagera Farmers Cooperative Bank, Mbinga Community Bank Limited, Meru Community Bank Limited, Njombe Community Bank Limited na FBME Bank Limited.

"Baadhi hawajaja kwa kuwa kiwango ni kidogo ikilinganishwa na maeneo wanayotoka na wengine taarifa hazijawafikia kuwa benki ikifungwa kuna utaratibu wa kupata fidia, tunawaomba kokote waliko waje kuchukua fedha zao," alisema.

"Tunawaomba wateja hawa watambue kuwa inapofungwa benki, serikali kwa mujibu wa sheria, imeweka utaratibu watu watapewa fidia na kwa utaratibu watu zaidi ya asilimia 90 wanakuwa hawajapoteza chochote. Kiwango cha Sh. milioni 1.5 ni baada ya kufanya uchambuzi wa waliokuwa na amana," alifafanua.

Alisema kiwango kinacholipwa ni kuanzia Sh. moja hadi milioni 1.5 na kama amana imezibakiza, atasubiri utaratibu wa kufilisi mali na kukusanya madeni ya benki husika.

Malisa alisema walianza na Sh. 250,000 mwaka 1994 na mwaka 2003 wakafika 500,000 kisha baadaye Sh. milioni 1.5 ambayo hulipwa kwa idadi ya amana na si idadi ya akaunti alizokuwa nazo mteja na kinachofanyika zinakusanywa kwa pamoja.

"Tunaposema asilimia 90 hawatapoteza chochote ni wale ambao wana kiwango cha chini ya Sh. mil 1.5 wanalipwa chote isipokuwa walio na zaidi ya kiwango hicho," alisema.

Alisema wenye fedha nyingi watasubiri ufilisi ambao hufanywa na mfilisi ambaye ana wajibu wa kuuza mali na kukusanya madeni na kuuza ili kinachopatikana kigawanywe kwa waliokuwa wanaidai benki kwa kiwango kinachozidi Sh. milioni 1.5.

Malisa alisema kwa sasa kinachofanyika ni kuuza madeni na kuuza mali za benki hizo, ili fedha zipatikane na kuwalipa wateja.

# Utafiti wabaini ukatili dhidi ya watoto shuleni

**Na Zuwena Shame**

ASILIMIA 17 ya watoto walioko shule za umma na asilimia 14.3 shule binafsi wamewahi kunyanyaswa kingono angalau mara moja, imefahamika.

Wakati hayo yakitokea, imefahamika kuwa asilimia 34.3 ya watoto wa shule kwa ujumla, wamenyanyaswa kisaikolojia hasa na wazazi au walezi kwa mwaka 2019 pekee.

Hayo yalibainika jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa ripoti ya utafiti unaohusu 'Hali ya Ukatili Dhidi ya Watoto wa Shule Tanzania Bara', ambao ulifanyika mwaka 2019.

Akizungumza baada ya uzinduzi wa ripoti hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kallaghe, akisema ili kutimiza ndoto za watoto kwa kusoma na kuishi kwenye mazingira salama na rafiki, jitihada za pamoja zinahitajika baina ya serikali na wadau mbalimbali katika kuondoa vyanzo vya ukatili na unyanyasaji.

Utafiti ulikuwa wenye lengo kuu la kupata taarifa rasmi na kujifunza hali halisi kuhusu ukatili na unyanyasaji dhidi ya watoto shuleni, pamoja na kuelewa vyanzo vya ukatili huo na kuboresha ulinzi na usalama wa watoto walio shuleni Tanzania Bara.

"Sisi sote kwa pamoja tunawajibu wa kutafuta ufumbuzi na kushughulikia sababu za unyanyasaji huu shuleni na nyumbani ili kuhakikisha watoto wanalelewa kwenye mazingira salama," alisema.

Dk. Kallaghe alisema ili kufanikisha malengo kuhakikisha watoto wanasoma katika mazingira salama, inapasa jamii na wadau mbalimbali kuelewa maana au dhana ya unyanyasaji au ukatili dhidi ya watoto, ambayo imekuwa na tafsiri tofauti kwenye jamii na kila mtu anauelewa tofauti kutokana na misimamo yake kidini, maadili, malezi au elimu.

Kutokana na utafiti huo, alisema HakiElimu imependekeza kuwapo namna ya kuingiza kwenye mitaala ya vyuo vya ualimu mafunzo ya ulinzi wa mtoto na udhibiti wa ukatili dhidi ya watoto ili walimu wanaohitimu wawe na uelewa na jinsi ya kuwalinda.

Pia HakiElimu imependekeza kuwa serikali inapaswa ihakikishe kuwa shule zote zina wafanyakazi wenye ujuzi wa taaluma ya ushauri elekezi na vilevile sheria na sera zilizopo, hasa Sheria ya Elimu ya Mwaka 1978 Sura ya 353 na marejeo ya mwaka 2002 na Kanuni za Utoaji Viboko Shuleni ya Mwaka 2002 zinazozungumzia masuala mbalimbali ikiwamo adhabu za viboko shuleni.

"Sheria inazitaka shule zote ziwe na kanuni ya nidhamu, lakini kwa bahati mbaya wakati wa kukusanya taarifa ya utafiti huu, shule nyingi zilibainika kutokuwa na kanuni hizo.

"Ni matumaini yetu kuwa kanuni hizi zitapendekeza na kusisitiza adhabu mbadala au nidhamu chanya alisema.



Ofisa Msimamizi wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Makao Makuu, Dinah Lwaga, akimwelimisha mfanyabiashara Samwel Meshack, wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi katika Halmashauri ya Mji Mdogo wa Makambako mkoani Njombe jana. P**ICHA: VERONICA KAZIMOTO**

# Waziri ashangaa hati nne miezi minane

**Na Munir Shemweta,**
SONGEA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameelezea kukerwa na Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma kutokana na kuandaa hati za ardhi nne katika kipindi cha miezi minane.

Pia Dk. Mabula ameonyesha kutoridhishwa na kasi ya utoaji hati katika halmashauri zote za mkoa wa Ruvuma, kwa kuwa katika kipindi cha miezi minane tangu kuanzishwa kwa ofisi ya ardhi ya mkoa, halmashauri zimeandaa hati 623 pekee.

Akizungumza na watendaji wa sekta ya ardhi na wakurugenzi wa halmashauri za mkoa wa Ruvuma juzi, katika kikao kazi cha kuzungumzia masuala ya ardhi na kuhamasisha ulipaji kodi ya pango la ardhi, Dk. Mabula alisema haiingii akilini halmashauri kuandaa hati nne kwa miezi minane, huku halmashauri ikiwa na watendaji wanaolipwa mishahara.

Katika kuhakikisha halmashauri za mkoa wa Ruvuma zinaongeza kasi ya utoaji hati, alisema ni lazima wakurugenzi kuwawekea malengo watendaji wa sekta ya ardhi kuandaa hati zisizopungua tatu kwa wiki kwa kila mtumishi.

"Uandaaji hati ufanywe na watendaji wote wa sekta ya ardhi kwa kupeana malengo ya kila mtumishi aandae hati ngapi. Kwenye halmashauri mtumishi anaweza kuanza na kuandaa hati tano au tatu 5 kwa wiki na mkifanya hivyo mnaweza kuandaa hati nyingi," alisema.

Taarifa ya sekta ya ardhi katika mkoa wa Ruvuma iliyowasilishwa na Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa, Ildefonce Ndemela, ilisema hati 623 ziliandaliwa na halmashauri za mkoa wa Ruvuma tangu kuanzishwa ofisi ya ardhi mkoa Machi, mwaka jana.

Alitaja idadi ya hati zilizoandaliwa kwa kila halmashauri kuwa ni Mbinga (52), Mbinga Mji (153), Manispaa ya Songea (2490, Namtumbo (nne), Madaba (16), Songea (34), Nyasa (82) na Tunduru (33).

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, baadhi ya halmashauri katika mikoa mingine zimekuwa zikifanya vizuri katika kuandaa hati na halmashauri mmoja huandaa hati 300 kwa mwezi. Alitolea mfano wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela katika mkoa wa Mwanza kuwa imekuwa ikiandaa hati 300 hadi 350 kwa mwezi.

Dk. Mabula aliziagiza idara za ardhi katika halmashauri za mkoa wa Ruvuma kuhakikisha zinampatia taarifa ya utekelezaji maagizo aliyoyatoa, yakiwamo makusanyo ya kodi ya pango la ardhi, ufuatiliaji wadaiwa sugu wa kodi ya pango la ardhi na utoaji wa hati za ardhi.

Katika hatua nyingine, Dk. Mabula alionyesha kutoridhishwa na hali ya makusanyao ya kodi ya pango la ardhi kwa mkoa wa Ruvuma. Hadi sasa, mkoa huo umekusanya Sh. 740,775,023 sawa na asilimia 16 ya malengo ya kukusanya Sh. bilioni 4.6.

# Taasisi za dini kutumika upimaji VVU

**Na Elizabeth Zaya**

TUME ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (TACAIDS), Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi Tanzania (NACP) kwa kushirikiana na wadau likiwamo Shirika la Misaada la Marekani (USAID) kupitia programu yake ya 'Tulonge Afya Leo', wamezindua machapisho ya kuhamasisha kupima Virusi vya Ukimwi (VVU).

Mpango huo unalenga kufanya uhamasishaji kupitia kwenye taasisi za dini hususani katika eneo la upimaji, na huduma zinazotolewa kwa wanaobainika kuwa na VVU.

Mkurugenzi Mtendaji wa TACAIDS, Dk. Leonard Maboko, alisema wanaamini kwamba viongozi wa dini ni rahisi kufikisha ujumbe katika jamii kwa sababu wanasikilizwa na kuaminiwa zaidi.

"Uzinduzi wa machapisho haya unalenga kuziwezesha taasisi za dini na viongozi wake, kuwa na taarifa sahihi kuhusu maambukizi, upimaji na matibabu ya VVU, kuboresha utoaji wa jumbe kwa waumini lengo likiwa ni kuhakikisha wanatambua afya zao na kupatiwa huduma kwa wakati muafaka," alisema Dk. Maboko.

"TACAIDS Tanzania inatambua mchango unaotolewa na taasisi za dini hapa nchini katika mapamba no dhidi ya VVU na Ukimwi, kwa kuweka mazingira wezeshi kwa wananchi kupata huduma za maambukizi ya virusi kwa taarifa sahihi."

Aliongeza kuwa mkakati uliopo kati ya Tume hiyo, taasisi za dini na wadau wanaofanya kazi katika afua mbalimbali ni kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo na kuudhibiti ifikapo mwaka 2030.

Mwakilishi wa taasisi za dini kwenye uzinduzi wa machapisho hayo ambaye ni Katibu Mkuu wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Nuhu Mruma, alisema machap isho hayo yamekuja kwa wakati muafaka.

# Ndulu azikwa, Gavana BoT afichua waliyoteta

**Romana Mallya na Joseph Baltazari**

MWILI wa Gavana wa zamani wa Benki Kuu (BoT), Profesa Benno Ndulu, umezikwa huku mrithi wake, Profesa Florens Luoga, akianika walivyoteta muda mfupi baada ya kuteuliwa kushika nafasi hiyo nyeti.

Profesa Ndulu, mtaalamu wa uchumi anayeheshimika kimataifa, alifariki dunia Dar es Salaam mapema wiki hii na mwili wake ulizikwa jana jijini.

Wakati wa misa ya kuuaga mwili wa Prof. Ndulu iliyofanyika Kanisa la Katoliki la St. Peters jana, Profesa Luoga alisema kuwa baada ya kuteuliwa na Rais John Magufuli, Prof. Ndulu alimpigia simu akiwa kitandani anaumwa na kumhakikishia kumsaidia katika nafasi hiyo.

"Prof. Ndulu alikuwa kitandani hospitalini nchini Marekani akiwa amefanyiwa upasuaji mkubwa, lakini alinipigia simu siyo kunipongeza, alinipigia kunitia moyo nisihofu, kazi nitaiweza na aliniambia atahakikisha ninaifanya kwa umahiri. "Kilichofuata kilinishangaza. Siku ya pili asubuhi, nililetewa begi lenye vitabu muhimu na Prof. Ndulu, alinitaka nianze kuvisoma ili nijue majukumu yangu ili tutakapokutana baada ya kupona, niweze kumwelewa katika mwongozo atakaonipa.

"Kweli, nilipokea begi lile, nilisoma vitabu vile. Alipopona, alirudi nilikaa naye, tukaongea, akaniambia pamoja na kwamba mimi ni mwanasheria, baada ya muda mrefu nitapaswa kuelewa uchumi na namna gani ya kuendesha Sekta ya Fedha ya nchi," alisimulia.

Profesa Luoga alisema mtangulizi wake huyo alimhakikishia kuwa mradi yuko hai, asisite kwenda kumuona na kumshirikisha kama kuna jambo litampa ukakasi katika majukumu yake hayo.

Alisema Benki ya Dunia (WB), Chuo cha Oxford na viongozi wakuu wa nchi za Afrika Kusini na Ethiopia waliendelea kumtumia. "Tutaendelea kumuenzi kama tutakavyokubaliana ndani ya benki ili. Maisha yake yaendelee kuwa na manufaa kwa vijana tunaowakuza ili waweze kuwa na elimu inayotakiwa kuweza kuhudumia taifa, kifo chake na jina lake litaendelea kubaki," alisema.

Akisoma salamu za rambirambi kutoka kwa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, Profesa Luoga alisema: "Nimeguswa sana na msiba wa mwalimu wangu, Prof. Ndulu. Nilipenda sana kushiriki kumuaga lakini kutokana na afya yangu nimeshindwa. Ninamwombea kwa Mungu apumzike kwa amani pamoja na ujumbe huu."

Alisema tangu kutokea kwa kifo hicho, amepokea salamu kutoka WB, Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), Uholanzi, Afrika Kusini, Lesotho, Namibia, Zimbabwe, Botswana, Msumbiji, Malawi, DRC, Zambia, Kenya, Rwanda, Burundi, Sudan Kusini na Uganda.

# Wanaotibu kienyeji magonjwa yasiyo ya kuambukiza waonywa

**Mwandishi Wetu**

WANAOUGUA magonjwa yasiyoambukiza (NCD) wameonywa kuwa katika hali mbaya zaidi hata kupoteza maisha iwapo watakuwa wanajitibu kwa waganga wa kienyeji.

Hayo yalisemwa juzi na mwelimishaji wa NCD kutoka Shirikisho la Vyama vya Magonjwa Yasiyoambukiza (TANCDA), Elizabeth Licoco, kwenye mafunzo kwa zaidi ya wagonjwa 40 kutoka kliniki za kisukari za hospitali za Temeke, Amana, Mwananyamala na Vijibweni, Dar es Salaam.

"Dawa zingine za asili zinapigiwa debe ni kama chakula lakini ukweli zina sumu nyingi na watumiaji wengi badala ya kutatua matatizo, wanajikuta wanajiingiza kwenye adha zaidi ya magonjwa kama vile ya figo, ini na hatimaye kuzidiwa hata kupoteza maisha," alionya Licoco.

Licoco alisema ana uzoefu wa zaidi ya miaka 25 wa kuhudumia wagonjwa katika kliniki za NCD hospitalini mkoani Dar es Salaam, ikiwamo Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na katika uzoefu huo, amebaini wengi waliozidiwa na hata kufa mapema ni wale waliojikita katika kutumia dawa za asili.

Alisema katika kuwafuatilia wagonjwa wake ambao walivutiwa na maneno mazuri ya matangazo ya dawa za asili kuwa hazina kemikali na ni kama chakula, alibaini walikufa mapema.

"Wengi wamekufa lakini hata leo nikienda pale Muhimbili nawakuta wengi niliokuwa nao bado wako vizuri na wanaendelea kuhudhuria kliniki kwa sababu tu wanafuata maelekezo ya wataalamu," alisema Licoco.

Alisema kwa sasa TANCDA inaweka mkakakati wa kuhamasisha wagonjwa kuwa na mazoea ya kukaa pamoja ili kuelimishana na kubadilishana uzoefu na kwamba kujua kwa undani ugonjwa unaomsumbua mtu, kunakuongezea maarifa na mbinu za kukabiliana nao.

NCD, alisema ni magonjwa yasiyo na vimelea vinavyoweza kuyasambaza na njia nzuri ya kuyadhibiti ni kwa kutumia mtindo bora wa maisha kama vile namna ya ulaji, kushughulisha mwili, kuwa na uzito sahihi na kudhibiti msongo wa mawazo.

Miongoni mwa magonjwa ya NCD ni kisukari, magonjwa ya moyo na mishipa ya damu, maradhi sugu ya njia ya hewa, matatizo ya akili, meno, saratani na yale ya kurithi kama vile siko seli.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, akionyesha vifaa vya hospitali kwa Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), Prof. Raphael Chibunda (kushoto), vilivyotolewa na benki hiyo, kwa chuo hicho wakati wa uzinduzi wa tawi la NMB SUA, mkoani Morogoro jana. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Raslimali Watu wa benki hiyo, Emmanuel Akoonay. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watoto wenye jinsia tata wafanyiwa upasuaji

**Na Christina Mwakangale**

WATOTO wanne waliozaliwa na jinsia tata, wamefanyiwa matibabu ya upasuaji katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), akiwamo aliyeishi na hali hiyo kwa miaka 15.

Bingwa wa Upasuaji Watoto katika hospitali hiyo, Dk. Zaituni Bokhary, akizungumza kuhusu suala hilo, alisema kuna ongezeko la watoto wanaozaliwa na jinsia tata, ambao baadhi yao hufika kliniki kwa ajili ya matibabu.

Alisema familia zilizo na watoto wa aina ambao kitaalamu hufahamika kama 'Ambiguous genitalia', huupata tafsiri tofauti kwenye jamii na kuwafanya kutokubali au kufanyiwa matibabu.

Alibainisha dhana potofu iliyopo kwa baadhi ya wanajamii na kufanya wazazi wenye watoto hao kuhofia kuwafikisha hospitalini watoto wao. Dk. Bokhary alisema kati ya watoto hao walifika MNH na kupatiwa matibabu, alikuwapo mwenye miaka sita, 15 na mwenye miaka 30.

Alisema mtoto mwenye umri wa miaka 15, anayesoma kidato cha tatu, ambaye alilelewa kama mtoto wa kiume aligundulika kuwa ni wa kike baada ya kubalehe. "Wazazi walipoona mtoto anapata siku zake akiwa na miaka 15, waliogopa kama pengine mtoto wao ana saratani, walipofika hapa hospitaini baada ya vipimo tukagundua ana mayai na ni mwanamke, ingawa alilelewa kiume," alisema Dk. Bokhary na kuongeza:

"Sasa yupo kidato cha tatu, alilelewa kama wa kiume, alipoanza kupata hedhi, wazazi walishtuka, tulibaini ni mtoto wa kike ingawa maumbile yake yaliwafanya wazazi kumuona ni wa kiume.

"Mtoto mmoja ambaye alilelewa kama wa jinsia ya kike, akatobolewa masikio, akavalishwa heleni alikuwa na malezi ya kike kwa miaka sita, alivyofikishwa hapa MNH tulimbadilisha kwa upasuaji sasa ni wa kiume, na anasoma darasa la nne hivi sasa," alisema Dk. Bokhary.

Dk. Bokhary alisema kati ya walio na tatizo hilo, alikuwapo mtu mzima ambaye ana miaka 29, alilelewa kiume, sasa ana miaka 32, aligundulika ni wa jinsia ya kike. "Huyu alikataa kubadilishwa, alisema ameshakuwa mtu mzima kwenye jamii ataonekanaje, kwamba amezoeleka wa kiume, anavaa nguo za kiume, ila ndani tuligundua ana matiti, anaingia kwenye siku zake," alisema bingwa huyo.

"Huyu kwa miaka 29 alikuwa anaishi kiume, alikuwa anaingia katika siku zake, ila aliona bora aendelee kuwa baba kuliko kuanza kuzaa, yaani kubeba mimba kwa sababu alikuwa na mayai ya kumwezesha kubeba ujauzito," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mabadiliko Halmashauri Jiji Dar yaje na ubunifu

**RAIS** John Magufuli juzi alitangaza kuivunja Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kuipandisha hadhi Manispaa ya Ilala kuwa Halmashauri mpya ya Jiji la Dar es Salaam.

Tunaipongeza Ilala kuwa Halmashauri ya Jiji, na hiyo ni hatua nzuri ambayo hata viongozi wenyewe na wakazi wa halmashauri hiyo watakuwa wameifurahia, lakini sasa hawanabudi kuongeza kasi katika utendaji wao.

Pamoja na kufurahia kupata hadhi hiyo adhimu, tuwakumbushe kuwa halmashuari ndiyo kitovu cha maendeleo ya wananchi, hivyo suala la ukusanyaji wa mapato kwa ajili ya huduma za jamii ikiwamo afya, elimu na nyingine ni la muhimu na kipaumbele.

Kwa maana hiyo, ukusanyaji mapato pia unahitaji kuchukukuliwa kwa umakini kwa kutumia sheria zilizopo na ndogondogo za halmashauri ili kuepuka kusababisha madhara kwa watu. Angalizo letu kwa madiwani ni kusimamia utekelezaji likiwamo suala la ukusanyaji wa mapato badala ya kujikita kwenye vikao tu na kugawana posho na kusahau maendeleo.

Dar es Salaam ilikuwa na manispaa tano, lakini Ilala imechaguliwa kuwa jiji, hiyo ni heshima ambayo Ilala yenyewe inatakiwa kuilinda, kwa kuongeza kasi, ubunifu wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa mapato na utoaji wa huduma kwa wananchi kwa tija na ufanisi.

Halmashauri hiyo ijipange kuweka mipango madhubuti na endelevu ambayo itaiwezesha kuendelea kukusanya mapato mengi zaidi ili kuiwezesha kutoa huduma mbalimbali zikiwamo za kijamii.

Tunaamini kwamba Ilala kuwa Halmashauri ya Jiji si kwa bahati mbaya, bali imekidhi vigezo vyote hususani makusanyo ya mapato kama Rais John Magufuli alivyoeleza jana katika siku ya pili ya ziara yake ya siku tatu mkoani Dar es Salaam.

Tunawakumbusha viongozi (madiwani na watendaji) kwamba jukumu kubwa lililoko mbele yao ni kuboresha jiji na kuliwezesha kufanya mambo makubwa hasa kwa kuzingatia kwamba, Dar es Salaam kwa sasa ni jiji la kibiashara.

Hivyo sasa ni wakati wa viongozi wa jiji hilo hilo kuongeza ubunifu katika kuibua miradi mipya na kutekeleza iliyopo pamoja na ukusanyaji wa mapato, ili liweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Kabla ya kuwa jiji, Ilala ilikuwa inatajwa kuwa miongoni mwa manispaa ambazo zinakusanya vizuri mapato, hivyo kwa uzoefu huo, ni wazi kwamba viongozi wakiongeza ubunifu, itakuwa rahisi jiji kupaa zaidi na kuwa mfano nchini.

Vilevile, tunaamini kwamba kuwapo kwa mabadiliko hayo, kuna faida nyingi, kwani hakutakuwa na Baraza la Madiwani la Jiji la Dar es Salaam, ambao wanateuliwa kuwakilisha manispaa.

Hii ina maana kwamba, madiwani wa Ilala, wataunda baraza lao, hivyo kupunguza gharama za uendeshaji ikiwamo mishahara, posho na pia kuondoa mgongano wa mamlaka katika usimamizi wa vyanzo wa mapato kati ya jiji na manispaa uliokuwapo kabla ya uamuzi wa juzi.

Tinaona pia kwamba kundi hilo litatengewa maeneo rasmi ya kufanya biashara katika mazingira rafiki, tofauti na ilivyo sasa.

Wakijengewa masoko ya kutosha na yenye miundombinu yote muhimu, itakuwa ni rahisi wao kwenda kufanya biashara na kuchangia kwa uhakika pato la jiji na hata taifa kwa ujumla.

Tunambua kuwa halmashauri hujiendesha kutokana na vyanzo mbalimbali vya mapato ambavyo hukusanywa, ndiyo maana tunasisitiza ubunifu ikiwamo kubuni vyanzo zaidi vya mapato, ambavyo hata hivyo, havitawaumiza wananchi.

Ni matarajio yetu kwamba Rais kama kiongozi mwenye dhamana na TAMISEMI, ataendelea kufanya maamuzi ya kuzipandisha hadhi halmashauri ambazo zitaonekana kupiga kasi katika suala zima la ukusanyaji mapato, badala ya kuzipandisha hadhi kwa sababu za kisiasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mamalishe na babalishe uvaaji kofia muhimu katika biashara

Na Sabato Kasika

**MAMALISHE** na babalishe wamejipatia umaarufu katika biashara yao, kutokana na kuuza chakula kwa bei ya chini inayoendana na uwezo wa kiuchumi wa wateja wao wa kutomudu kununua chakula cha bei ya juu.

Ni biashara iliyoshamiri katika maeneo mengi nchini na hasa mijini. Imekuwa ni ajira inayowafanya wajikimu kimaisha, ikiwamo kulisha familia na kusomesha watoto wao.

Hata hivyo, kuna kosa ambalo baadhi yao wanalifanya, ambalo ni vyema mamlaka husika zikalitafutia ufumbuzi wa kudumu ili biashara hiyo iweze kufanyika kwa ufanisi zaidi bila athari zozote za kiafya kwa wateja.

Ni suala la baadhi ya mamalishe na babalishe kutovaa kofia, hali inayoweza kusababisha nywele kudondokea katika vyakula na kuleta madhara kiafya kwa wateja.

Kwa kuwa ni muhimu katika uandaaji vyakula, pia ni vyema wahusika wakaelimishwa umuhimu wa kuvaa kofia, hata vitambaa maalum vifuani viitwavyo 'apron'.

Nakumbuka, yapo baadhi ya maeneo jijini Dar es Salaam, ikiwamo Mikocheni na Viwandani, mamlaka husika hasa manispaa, ziliwahi kugawa kofia kwa mamalishe, lakini kwa sasa hawavai.

Haijulikani ni kwa nini? Sijui zimechakaa, au ni uzembe tu na kama zimechakaa, kwa nini wasishone mpya ama kuvaa hata vitambaa ili kulinda afya za wateja wao?

Kama hawajui umuhimu wa kuvaa kofia wanapokuwa katika biashara hizo, tena wateja wengi ni wa kipato cha kawaida, basi ni wajibu kwa mamlaka husika kuwapa elimu.

Kuvaa kofia si kwa afya za wateja tu, bali wanajilinda hata wenyewe. Hivyo, kuwapa elimu za kuzivaa ni jambo muhimu na linaweza kuwasaidia kuboresha biashara zao.

Binafsi huwa nimaamini, hilo liko ndani ya uwezo wao. Niseme, kuna tatizo lingine linalowakabili la ukosefu wa maeneo ya kufanya biashara, hali inayosababisha 'wavamie' hata pasikoruhusiwa.

Kukosa maeneo rasmi ya kufanya biashara, inasababisha waingie katika orodha ya wanaochafua mazingira, kwa kuwa wanakosa mahali pa kutunza taka wanazozalisha katika biashara zao.

Sasa kuna utamaduni fulani unaojengeka kimyakimya, unamkuta mamalishe na babalishe wakimwaga maji waliooshea vyombo vyao na makombo ya vyakula katika mitaro au eneo lolote la wazi.

Wanafanya hivyo, kwa kuwa hawana sehemu ya kutunzia takataka, hawako katika maeneo rasmi ambayo yangekuwa na huduma zote za muhimu kwao na hata kwa wateja wao.

Pia katika mazingira hayo ya ukosefu wa maeneo ya kufanyia biashara, wanajikuta mvua na jua vyao, kutokana na kwamba hawawezi kujenga vibanda vya kudumu, katika maeneo ambayo si rasmi kwa biashara.

Hivyo, njia mojawapo ya kuwasaidia, ni mamlaka husika kuwatengea maeneo rasmi ili wafanye biashara yao katika mazingira safi, huku pia wakizingatia usafi ikiwamo kuvaa kofia.

Ninaamini, Watanzania wengi wanapenda kula kwa mamalishe na babalishe, kutokana na ukweli kwamba, wanauza vyakula vyao kwa bei ambayo inalingana na uwezo wao wa kiuchumi.

Kukiuka kanuni hizo za afya na mazingira, inabebesha maana kwamba, iwapo wataboreshewa mazingira ya biashara, lakini wakaendelea kutozingatia usafi ikiwamo kutovaa kofia na kutupa takataka ovyo, basi hilo litakuwa ambalo ikibidi zichukuliwe hatua za kisheria.

Hili la sasa kina mamalishe na babalishe katika kusaka riziki, wanashughulika pasipokuwapo choo wala maji, sasa wao na wateja wanajisitiri wapi? Wanajua wenyewe!

Tunafahamu, ili wawe na huduma, sharti kuwatengea mahali penye wateja wengi, kwani upande wa pili ni hao ni wale wapigakura wa mkuu wetu Rais John Magufuli, aliyotamka juzi pale siku ya mwisho kabla ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam 'kutumbuliwa' na kwa lugha ya kijeshi Manispaa ya Ilala 'imekaba lofu' nafasi yake, muda mfupi baada ya kupata mtoto.

'Stendi ya Kimataifa ya Mbezi Luisi.'

Ni vyema kila halmashauri zote nchini, zikaangalia uwezekano wa kuwasaidia wafanyabiashara hao ili waboreshe huduma zao, badala ya kuendelea kuzifanyia katika mazingira yasiyofaa.

Asanteni.

# ATCL yarejesha safari za Songea

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

SHIRIKA la Ndege la Tanzania (ATCL), limerejesha safari za ndege mkoani Ruvuma baada ya kukamilika ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Ruhuwiko, mjini hapo.

Serikali ilitoa zaidi ya Sh. bilioni 37 kukarabati uwanja huo na kuwezesha ndege aina ya Bombardier Q400 kuanza tena safari zake za kuruka na kutua kuanzia Februari 17, mwaka huu.

Akizungumza jana baada ya kushuka katika safari ya kwanza ya Bombadier kwenye uwanja wa Songea, Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye ni Mbunge wa Songea Mjini, Dk. Damas Ndumbaro, alisema kuanzishwa kwa safari hizo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM.

"Ibara ya 58 ya Ilani ya CCM imetamka kwamba Uwanja wa Ndege wa Songea utajengwa. Ilani imetamka kwamba zitanunuliwa ndege 11 mpya na kwamba ATCL itaongeza safari za ndege kutoka viwanja vinne mwaka 2015 hadi viwanja 13 mwaka 2021. Songea ni kiwanja cha 13," alisema Ndumbaro.

Alisisitiza kuwa Uwanja wa Ndege Songea utafungua anga la mkoa wa Ruvuma na kuruhusu wawekezaji na watalii kufika Ruvuma kujionea fursa mbalimbali za uwekezaji na utalii, hivyo kuchangia pato la taifa na kuinua uchumi wa wananchi wa mkoa wa Ruvuma na taifa kwa ujumla.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Pololet Mgema, alimpongeza Rais kwa kutoa fedha ambazo zimekamilisha ujenzi na ukarabati wa uwanja huo ambao umeanza kutumika rasmi kutua ndege kubwa.

Naye Meneja wa Uwanja wa Ndege Songea, Jordan Mchami, alisema safari za ndege za ATCL zimerejeshwa mkoani Ruvuma na kwa kuanzia, safari toka Dar es Salaam hadi Songea zitakuwa Jumatano na Jumapili.

Uwanja wa Ndege wa Songea ni miongoni mwa viwanja bora vya ndege Tanzania. Ulijengwa kati ya mwaka 1974 na 1980 na uliwekewa lami hivyo kuwa na uwezo wa kutua ndege majira yote masika na kiangazi.




Waziri wa Madini, Dotto Biteko (wa pili kushoto), akimsikiliza Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Dhahabu ya Barrick, Mark Bristow (wa pili kulia), alipokaribishwa katika kikao kazi cha watendaji wa kampuni hiyo, jijini Mwanza jana, kujadili mikakati mbalimbali ya kuifanya kampuni ya Twiga Mineral, inayomilikiwa kwa ubia wa Barrick na Serikali ya Tanzania, kuendelea kufanya vizuri katika migodi yake ya North Mara, Buzwagi na Bulyanhulu. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kibano chaja kwa wafugaji, wakulima uharibifu barabara

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

BAADHI ya wajumbe wa Bodi ya Barabara mkoani Rukwa, wamewalaumu wafugaji na wakulima kuwa wamekuwa chanzo cha kuharibika barabara na madaraja kutokana na shughuli wanazozifanya.

Lawama hizo walizitoa jana walipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa daraja la Mto Kankwale linalojengwa kwa gharama ya Sh. milioni 238 na daraja la Mto Momoka linalojengwa kwa gharama ya Sh. 270 katika Manispaa ya Sumbawanga.

Mmoja wa wajumbe hao ambaye ni Mbunge wa Kalambo, Josephat Kandege, alisema shughuli za kibinadamu wanazofanya kiholela wakulima na wafugaji zimekuwa chanzo kikubwa cha kuharibika kwa miundombinu hiyo.

Alisema baadhi ya wakulima wamekuwa wakilima kwenye vyanzo vya maji, pembeni ya barabara na mito, kitendo kinachosababisha kutokea mmomonyoko wa ardhi unaosababisha madaraja mengi kusombwa na maji.

"Baadhi ya wakulima wamekuwa wakilima bila kufuata sheria ya mazingira, hivyo wanalima hadi pembeni ya mito wanasababisha mito kujaa udongo na kina kuwa kifupi, matokeo yake mito inapoteza uelekeo na maji kupita pembeni ya barabara na madaraja yanabomoka," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, ambaye ni mwenyekiti wa bodi ya barabara ya mkoa huo, alimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Sumbawanga kutumia sheria za mazingira na sheria ndogo za halmashauri kuwabana wakulima wanaolima karibu na vyanzo vya maji na pembeni mwa barabara.

Pia alimwagiza kuwachukulia hatua kali wafugaji wanaochunga mifugo yao kwenye vyanzo vya maji na pembeni mwa barabara, kwani mifugo imekuwa ni chanzo kikubwa cha kuharibu barabara na kusababisha ajali.

Mratibu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) mkoani Rukwa, Mhandisi Seth Mwakyembe, alisema daraja la Kankwale linajengwa kwa gharama ya Sh. milioni 238, lakini limeanza kumomonyoka udongo kabla ya ujenzi wake kukamilika, huku mkandarasi akiwa ameshalipwa Sh. milioni 167.3 wakati akitarajiwa kuukamilisha Jumapili.

# Balozi aiahidi kampuni ya machinjio masoko ya nje

**Na Beatrice Shayo**

BALOZI mdogo wa Tanzania nchini Dubai, Shabaan Khatib Baraza, ameiahidi kampuni ya machinjio ya kisasa na wauzaji wa nyama ya mbuzi, kondoo na ng'ombe nje nchi (TANCHOICE ) kuwasaidia kupata kibali cha kuuza bidhaa zao katika mataifa ya ughaibuni yakiwamo Falme za Kiarabu (UAE).

Alitoa ahadi hiyo, juzi, alipotembelea Maonyesho ya 26 ya Biashara za Bidhaa za Chakula (Gulfood 2021) ambayo hufanyika Dubai kila mwaka.

Alisema soko la bidhaa ya nyama kwa nchi za UAE ni kubwa, kwani taifa hilo linapenda nyama kutoka Tanzania kwa sababu ya uhalisia wa nyama zake pamoja na ladha.

"Naahidi kutoa ushirikiano kwenu zaidi ili muweze kupata kibali cha kuuza nyama au bidhaa katika nchi za Umoja wa Falme za Kiarabu, kwani soko lake linahitaji nyama ya Tanzania, na soko lake ni kubwa kwani nyama zake zinapendwa zaidi kwa radha ya uasili wake," alisema Balozi Baraza.

Meneja Mauzo wa TANCHOICE, Mussa Mushi, alisema ni mara yao ya kwanza kushiriki katika maonyesho hayo, na wameweza kujifunza vitu vingi kutoka katika mataifa mengine yanaouza bidhaa kama zao.

Alisema kupitia maonyesho hayo wamegundua kuwa nyama ya Tanzania inapendwa sehemu nyingi duniani, na kwamba wanapeleka bidhaa zao kwa nchi ya Oman na Kuwait.

Mushi alisema kwa mwezi wanapeleka tani 200 za nyama ya mbuzi na kondoo freshi katika nchi hizo ila soko kubwa lipo Dubai na Saudi Arabia, ambako hawajaanza kupeleka bidhaa zao sababu ya vibali.

"Tunafurahi kushiriki katika maonyesho haya na tumefurahi kuiwakilisha Tanzania, kwani inaonyesha ni namna gani nchi yetu imebarikiwa kuwa na idadi kubwa ya mifugo na yenye ladha nzuri," alisema.

# CTI, waziri kujadili uboreshaji viwanda

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKISHO la Wenye Viwanda nchini(CTI), linatarajia kukutana na Waziri wa Viwanda na Biashara, Geoffrey Mwambe, Machi mosi mwaka huu, kwa ajili ya kujadili mambo mbalimbali ya kuboresha sekta hiyo nchini.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa CTI, Leodeger Tenga, alisema lengo la kukutana naye ni kumweleza mambo mbalimbali ya sekta hiyo na kujadili namna ya kusukuma maendeleo ya viwanda nchini.

Tenga alisema, mambo mengine wanayotarajia kuyajadili ni pamoja na masuala ya kodi.

"Utaratibu ambao umewekwa hivi sasa ni kwamba kama wanachama wana mambo wanataka kuyajadili lazima wakutane na kuzungumza na kuyatafutia ufumbuzi, na kila mwaka tunakuwa na utaratibu wa kuchambua yale yanayotokea katika sekta hii, ili kupata maoni mbalimbali yakiwamo ya kikodi na kuyafanyia uchambuzi," alisema Tenga.

"Na lengo kubwa ni kwamba kuna vitu vingine ambavyo vinatakiwa kuzungumzwa na kutafutiwa ufumbuzi kupitia mijadala kama hii ili kutoa nafasi kwa viwanda vyetu vya ndani kufanya vizuri na kuleta ushindani, na mkutano huu utahusu washirika wote wa CTI pamoja na wengine wenye viwanda wasio wanachama."

Tenga alisema kama wenye viwanda na wazalishaji wakuu wa bidhaa, wako mstari wa mbele kuungana na serikali katika mipango yake ya kutumia viwanda kama mhimili wa uchumi na kuhamasisha matumizi ya bidhaa zinazozalishwa ndani ya nchi.

Alisema lengo lao ni kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi unaotokana na viwanda vya ndani kuzalisha bidhaa za ushindani mkubwa katika mauzo ya nje.

"Kama mnavyofahamu kipindi cha miaka mitano iliyopita imepita kwenye dhana ya ujenzi wa Tanzania ya viwanda na tunafahamu mafanikio ambayo yamepatikana kiasi cha kufikia uchumi wa kati kabla ya muda uliokuwa unatarajiwa, na kipindi kinachokuja ndio hicho hicho, kwamba tunataka uchumi ambao unategemea mauzo ya nje," alisema Tenga.

"Na mauzo hayo kwa kiasi kikubwa ni kwa kutegemea bidhaa zetu ambazo zimechakatwa ndani ya nchi yetu, kwa hiyo sisi wenye viwanda tunafurahia hiyo na tunashukuru kwamba serikali inatutegemea na tunaahidi kwamba tutalifanikisha hilo."

Aliwataka wenye viwanda kutumia fursa hiyo ili kuhakikisha wanashiriki na kuwasilisha maoni yao kwa waziri huyo mwenye dhamana ili yafanyiwe kazi.

# NHC sasa kuwasaka wadeni sugu kodi

**Na Munir Shemweta,**
SONGEA

SHIRIKA la Nyumba la Taifa (NHC) limewataka wapangaji wa nyumba zake wanaodaiwa kodi na kushindwa kulipa kutokana na sababu mbalimbali kufika ofisi za shirika hilo, ili kuangalia namna bora ya kufanikisha kulipa fedha wanazodaiwa kabla ya kuanza kuchukuliwa hatua za kisheria.

Meneja Huduma kwa Jamii wa NHC, Muungano Saguya, alisema hayo juzi, baada ya muda uliowekwa kwa wapangaji wanaodaiwa kodi za nyumba wawe wamekamilisha kulipa kufikia Januari 30, mwaka huu.

Wapangaji hao wanaodaiwa wameanza kuitikia wito huku wengine wakiwa bado hawajakamilisha kulipa malimbikizo wanayodaiwa.

Akizungumza mbele ya watendaji wa sekta ya ardhi na wakurugenzi wa halmashauri za Mkoa wa Ruvuma, wakati wa ziara ya Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, Saguya alisema ni vizuri wale wadaiwa wenye matatizo ya malipo wakaenda ofisi za shirika zilizoko kila mkoa na kuonana na watendaji wa shirika hilo ili kuangalia namna bora ya kulipa madeni yao kwa wakati.

Saguya alisema NHC ina zaidi ya nyumba 17,000 nchi nzima na hadi Januari, mwaka huu, ilikuwa linadai malimbikizo ya zaidi ya Sh. bilioni 27 kutoka kwa wapangaji ambao wamelimbikiza kodi yao.

"Tulitoa mwezi mmoja hadi tarehe 30 Januari wadaiwa wote wawe wameshalipa madeni ya kodi ya nyumba. Wale watakaoshindwa wataondolewa katika nyumba za shirika na kufikishwa katika vyombo vya sheria," alisema Saguya.

Alibainisha baada ya muda waliopewa wadaiwa sugu kwisha, shirika limeanza kufanya uchambuzi wa wadaiwa wote ili kubaini mwenendo wa ulipaji wa malimbikizo hayo na kazi hiyo itakamilika mwisho wa mwezi huuu na mwezi ujao, shirika litaanza kufuatilia wapangaji nyumba hadi nyumba ili kubaini walioshindwa kulipa na wale wenye changamoto ambazo shirika linaweza kukaa pamoja kutafuta ufumbuzi.

Kwa mujibu wa Saguya, nyumba za NHC ni za Watanzania wote, hivyo mpangaji anayeishi katika nyumba hizo, anapaswa kulipa kodi kwa wakati kwa lengo la kuliwezesha shirika kujiendesha.

Kwa kufanya hivyo, alisema shirika pia litalipa kodi mbalimbali za serikali, kuzifanyia matengenezo nyumba zake na kujenga nyumba mpya kwa ajili ya Watanzania wengine wasiopata fursa ya kupanga katika nyumba za shirika.

Meneja huyo pia alisema mbali na NHC kupangisha nyumba zake, imekuwa ikishiriki katika upangaji miji na ujenzi wa miradi mbalimbali ya kimkakati ikiwamo ujenzi wa hospitali za rufani za Mwalimu Nyerere mkoani Mara na ile ya Kanda ya Kusini mkoani Mtwara.



Waendesha pikipiki wakipita kwenye barabara iliyoharibika vibaya inayohitaji kukarabatiwa katika eneo la Chanika, jijini Dar es Salaan jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Waziri amsimamisha kazi mkuu ukaguzi wa mifugo

**Na Julieth Mkireri,**
CHALINZE

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amemsimamisha kazi Msimamizi wa Kituo cha Ukaguzi wa Mifugo Ruvu Darajani, Halmashauri ya Chalinze, Gabriel Lyakurwa, kwa tuhuma za upotevu wa mapato.

Gekul alitoa uamuzi huo, jana, alipokuwa katika ziara ya siku moja katika halmashauri hiyo kukagua ujenzi wa bwawa la mifugo Chamakweza na kuzungumza na wananchi.

Alisema msimamizi huyo wa kituo anasimamishwa kazi kupisha uchunguzi dhidi ya tuhuma zilizoelekezwa kwake.

Naibu Waziri Gekul alifikia uamuzi huo baada ya taarifa kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, msimamizi huyo anavyotuhumiwa kugeuza kituo hicho cha ukaguzi kuwa cha kupitisha mifugo kwa njia za panya.

Pia amewataka maofisa mifugo kujitathimini kama wanatosha kuendelea na kazi katika maeneo yanayolalamikiwa katika migogoro ya ardhi kati ya jamii ya wakulima na wafugaji.

Gekul alitoa maelekezo hayo akiwa katika vijiji vya Chamakweza, Ruvu Darajani na Kitonga.

Alisema maofisa hao katika Halmashauri ya Chalinze, wanatakiwa kujipima kama wanaweza kuendelea kuwapo baada ya kushindwa kutatua migogoro ya wakulima na wafugaji ambayo imedumu kwa muda mrefu.

Pia Naibu Waziri huyo alimtaka Mwenyekiti wa Halmashauri ya Chalinze kuangalia kama wajumbe wa kamati ya mipango miji wanatosha kuendelea kubaki madarakani kutokana na kushindwa kushughulikia migogoro iliyopo.

"Mwenyekiti wa Halmashauri unda kamati ndogo ya mipango miji. Nendeni maeneo yenye migogoro ongeeni na wananchi na kutafutia ufumbuzi ili shughuli zingine za kimaendeleo ziendelee," alisema.

Gekul alisema wizara hiyo imepokea migogoro 40 ikiwamo iliyoko katika Mkoa wa Pwani itahakikisha inafika mwisho na hakuna tena malumbano na kuwataka wenyeviti wa vijiji kuacha tabia ya uuzaji holela wa maeneo.

Kuhusu ujenzi wa bwawa la mifugo unaoendelea katika eneo la Vigwaza, alimtaka mkandarasi kulikamilisha mapema ifikapo Machi, mwaka huu, ili wafugaji waanze kulitumia.

Alisema wafugaji pia wazuie mifugo yao kufika kwenye maeneo ya ujenzi wa bwawa hilo kwa kuwa wanachangia kuchelewesha uwakilishaji kwa muda unaotakiwa.

Kuhusu mgogoro wa mipaka kati ya Pingo na Chamakweza, vijiji ambavyo wanaishi wakulima na wafugaji, alisema taratibu zinafuatwa na wizara hiyo inawaomba wananchi kuwa watulivu wakati ufumbuzi ukitafutwa.

# MPRU yapewa miezi 5 mipaka ya hifadhi

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, amekitaka Kitengo cha Hifadhi ya Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) kuhakikisha hadi kufikia Agosti mwaka huu kiwe kimeweka alama za mipaka katika maeneo yote ya hifadhi za bahari ili kuondoa migogoro kati yake na wavuvi.

Akizungumza na wananchi katika Kata ya Jibondo iliyopo Wilaya ya Mafia mkoani Pwani, Ndaki alitaka kuwekwa kwa alama za mipaka hiyo baada ya baadhi ya wananchi kulalamikia kutozwa faini mara kwa mara kwa madai ya kutuhumiwa kufanya shughuli za uvuvi kwenye maeneo hayo ambayo hayaruhusiwi kisheria kwa shughuli hizo.

Aliwataka wavuvi kuhakikisha wanapatiwa risiti za kielektroniki (EFD) wanapokamatwa kwa makosa mbalimbali ambayo ni kinyume cha sheria ya uvuvi na kuonya watumishi wa serikali wanaopokea fedha za faini bila kutoa risiti hizo.

Pia, Ndaki alitoa mwezi mmoja kuhakikisha kunafanyika utafiti kuhusu matumizi ya aina mbalimbali ya nyavu za uvuvi baada ya kupata malalamiko ya kuwapo kwa baadhi ya wavuvi kutumia nyavu haramu.

Alimtaka Katibu Mkuu Wizara hiyo anayeshughulikia Uvuvi Dk. Rashid Tamatamah, kuhakikisha ifikapo Machi 23, mwaka huu awe amempatia taarifa hiyo ili atoe mwongozo wa matumizi kuhusu nyavu zinazotakiwa katika shughuli za uvuvi.

Alipiga marufuku kwa baadhi ya Maofisa uvuvi ambao wamekuwa wakiwakamata wachuuzi wa samaki mitaani bila sababu za msingi.

"Kuna baadhi ya Maofisa wamekuwa wakienda masokoni kuwanyanyasa wakina mama wachuuzi wa samaki eti kwamba wanauza samaki ambao ni kinyume cha sheria, sitaki kuona kabisa mambo haya na iwe marufuku, kama ukiona kuna tatizo la namna hiyo kwa nini usiwaulize wakuambie aliyewauzia ili upate chanzo halisi?" alihoji Ndaki.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mafia, Juma Ali, alisema hatua iliyochukuliwa na serikali ya kusimamia maeneo ya hifadhi ya bahari ni muhimu na itasaidia kutatua baadhi ya matatizo ambayo yamekuwa yakijitokeza.

Alisema matatizo ambayo yamekuwa yakitokea kutokana na kutokuwapo kwa usimamizi mzuri katika maeneo hayo Tengefu, yamekuwa yakizorotesha hali ya uhifadhi katika wilaya hiyo.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja (katikati), akieleza umuhimu wa kutoa elimu ya masoko kwa wanafunzi wanaosoma katika Chuo cha Taifa cha Utalii kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Shogo Mlozi (kulia), baada ya kikao na uongozi wa chuo jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Chuo cha Utalii chatakiwa kusimamia ubora wa elimu

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imekitaka Chuo cha Taifa cha Utalii Tanzania kusimamia taratibu na miongozo ya ubora wa elimu iliyowekwa ili kuwajengea uwezo wanafunzi wanaohitimu chuoni hapo kujiajiri wenyewe.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary masanja, alibainisha hayo alipokutana na Menejimenti ya Chuo hicho jijini Dar es Salaam.

Masanja alisema ni muhimu Chuo hicho kinapofundisha wanafunzi kiangalie namna ya kuwajengea uwezo wanafunzi hao kwenda kujitegemea. "Pia angalieni namna ya kupata masoko kwa ajili ya kuwashawishi watalii wa ndani na nje ya nchi waje kutalii hapa nchini," alisema.

Alisema pamoja na chuo hicho kutoa elimu ya masuala ya Utalii kinapaswa kufikiria namna ya kujitanua ili kuuza bidhaa zake na kuongeza mapato kupita utalii kwa muda mfupi.

'' Mnapaswa kujitangaza kupitia huduma mnazotoa, mnaweza kuona ni kituo kidogo lakini mnaweza kujikuta mmefika mbali zaidi,'' alisisitiza.

Alitoa wito kwa vijana wanaosoma masuala ya utalii chuoni hapo waweke bidii katika kujifunza na kuzifahamu lugha mbalimbali ili kuwasiliana vizuri na kuwahudumia watalii wanaokuja hapa nchini.

# Waeleza elimu ilivyopaisha mavuno ya kahawa

**Na Restuta Damian,** KAGERA

BAADHI ya wakulima wa kahawa kata za Mabira, Wilaya za Kyerwa na Kyebitembe Wilaya ya Muleba, mkoani Kagera, wameeleza jinsi elimu ya uchipulishaji mibuni shambani iliyosaidia kupata ongezeko la mavuno ya kahawa ya maganda.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, Jovinus Ishemba, mkulima Kata ya Kyebitembe; Philbert Kahabuka mkulima Kata ya Mabira; Marigoleth Kato walisema, kabla ya kupatiwa elimu hiyo kutoka kwa wataalamu mbalimbali waliokuwa wanatoa elimu ya uzalishaji bora imesaidia mavuno kuwa mengi.

Ishemba alisema baada ya kuelimishwa njia ya uchipulishaji ambayo binafsi imetumika kwa mwaka mmoja amepata mafanikio kwa kuvuna mavuno kuanzia kilo moja kwenye shina moja.

"Mapokeo ya elimu yamesaidia kutoka zama za awali kwenye mavuno kidogo na miche kutokuwa na ustawi kwa vile kulikuwa na mlundikano mwingi wa matawi kwenye shina moja bila kupunguza na kubakia na yanayotakiwa,"alisema Ishemba.

Kahabuka alisema, ongezo la mavuno ni njia ya kuandaa mashamba kabla ya kutaka kupanda na kufata taratibu za wataalamu.

Alisema, utunzaji wa miche ukiwa mdogo ambazo zinanunuliwa kutoka kwenye Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kituo chaTARI Maruku, mashirika na halmshauri ya wilaya umejenga uhusiano bora.

Kahabuka alisema, njia nyingine iliyokuwa inatumika ni kufanya mawasiliano ya wataalamu kuja shambani kuangalia tatizo na kulitatua na kuacha elimu endapo tatizo litajirudia tena.

"Nimekuwa nikitembea kwa watu wa Cafe afrika, TARI na Halmashauri, pia naenda kuomba msaada na kuwaomba wafike shambani hivyo hivyo na wengine wanaenda hadi unakuta elimu inaenea pote," alisema Kahabuka.

Meneja wa Shirika la uzalishaji miche na uchipulishaji mashamba ya mibuni mkoani Kagera, Daniel Mwakalinga, alisema elimu iliangalia eneo ambalo kuna uhitaji zaidi ambazo ni wilaya za Bukoba, Muleba, Kyerwa, na Karagwe, na kwamba imekuwa na manufaa ya mavuno ikilinganishwa na hapo awali.

Mwakalinga alisema, mategemeo yaliyopo ni kuondoa hali ya mkulima kuvuna nusu kilo na kufikia kilo moja kwa mche mmoja inayomnufaisha na kufanya apende kilimo.

# Wanaochelewesha miradi ya maji kukiona

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

SERIKALI imewaonya makandarasi wanaotekeleza miradi ya maji na kuwataka kufanya kazi usiku na mchana ili kuikamilisha, na kwamba watakayeshindwa serikali itavunja mikataba yao.

Hayo yalibainishwa jana jijini Mwanza na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi, wakati wa ziara yake ya kikazi ya kutembelea miradi ya maji iliyopo Nyamagana na Ilemela mkoani Mwanza Alisema lengo la ziara hiyo ni kuyafikia maeneo yenye miradi iliyosimama kwa muda mrefu ili kupata ufumbuzi ambao utasaidia upatikanaji wa maji kwa wananchi, hivyo makandarasi wazembe watakaochelewesha miradi serikali haitowavumilia.

Alisema serikali inafuatilia mikataba ili kujua masharti na vigezo ambavyo watavizingatia, na kwamba miradi hiyo itaendelea kusimamiwa na wataalamu wa ndani kupitia 'force' akaunti ili kukamilisha.

" Hakuna kuongeza muda labda yatokee mafuriko yatakayosababisha kusombwa kwa miundombinu hayo tutayazingatia, lakini kwa wale wasiokuwa na sababu hizo tutavunja hiyo mikataba," alisema Mahundi.

Alisema baada ya miaka mitano wananchi watapunguziwa kero za maji kwa maeneo ya mijini itakuwa zaidi ya asilimia 95 huku vijijini ikiwa asilimia 85 hadi sasa hali inaridhisha kwani miradi mingi miundombinu imefanyika kilichobaki ni umaliziaji.

Aliongeza kuwa maadhimisho ya wiki ya maji mwaka huu yanayofanyika mwezi ujao watahakikisha miradi mingi inatoa maji.

Aliwataka makandarasi kuharakisha miradi hiyo na kuacha mazoea ili kuyafikia malengo kwani sekta hiyo imejipanga kufanya mapinduzi na kuhakikisha maji yanatoka bombani.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MWAUWASA, Leonard Msenyele, alisema uzalishaji wa maji jijini Mwanza kupitia mtambo wa Kapripoint ni wastani wa lita milioni 90 kwa siku huku mahitaji halisi yakiwa ni lita milioni 150 kwa siku hivyo bado wanakabiliwa na upungufu wa takriban lita milioni 60 kwa siku.

Alisema mradi huo wa Nyamagana ambao unahusisha kupanua na kuboresha huduma za maji katika maeneo ya kusini na katikati la Jiji hilo unatekelezwa sambamba na ujenzi chanzo kipya cha Butimba ambacho kitazalisha lita milioni 48 kwa masaa 24 hivyo tatizo la upatikanaji maji litapungua .




Mkurugenzi wa Biashara Vodacom Tanzania Plc, Linda Riwa (kulia), akifafanua jambo kwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi. Andrea Mathew Kundo (kushoto mbele) na wajumbe wa kamati ya utendaji kampuni hiyo, na maofisa kutoka UCSAF, TCRA-CCC na TCRA, walipofanya ziara ya kikazi kwenye makao makuu ya Vodacom, Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam juzi, kwaajili ya kujenga uhusiano wa karibu kati ya serikali na tasnia ya mawasiliano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri azifunda taasisi elimu ya juu

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amezitaka taasisi za elimu ya juu nchini kuhakikisha wanazalisha wataalamu watakaoleta maendeleo, kwamba visiwe sehemu ya wanafunzi kufanya utalii.

Amevitaka kukaza 'buti' kuhakikisha wanazalisha wataalamu wengi wenye viwango vyenye ubora ambao wataliletea taifa sifa ndani na nje ya nchi.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akifanya uzinduzi wa ufadhili kwa kuzingatia kiwango cha juu cha ufaulu, unaotolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Prof. Ndalichako alisema: "Taasisi za elimu ya juu tunataka zitengeneze ama kuzalisha wataalamu watakaoleta maendeleo. Visiwe sehemu ya wanafunzi kuja kufanya utalii, tunataka mwanafunzi akimaliza masomo awe ameiva sawasawa".

Kuhusu uzinduzi wa program hiyo, Prof. Ndalichako alisema itakuwa ni fursa kwa Watanzania wote kupata ufadhili wa mosomo kutoka UDSM. Alisema UDSM kimekuwa chuo cha kwanza nchini kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa sekondari waliofanya vizuri.

"UDSM kimetumia mapato yake ya ndani kuendesha mfumo huu, nivitake vyuo vingine viige utaratibu huu kwani ni mzuri kwa maendeleo ya taifa," alisema.

Aidha, aliwataka wanafunzi wa elimu ya juu nchini kutumia vizuri uhuru wanaoupata wakiwa vyuoni, kwa kusoma kwa bidii, kwamba wasiendekeze starehe.

Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. William Anangisye, alisema utaratibu huo ulianza mwaka juzi kwa UDSM kuwasomesha wanafunzi waliopata ufaulu wa juu masomo ya sayansi kwa kidato cha sita.

Alisema UDSM ilitenga Sh. milioni 237 kwa ajili ya ufadhili wa program hiyo, kwamba mchakato wa kuwapata wanafunzi ni wa wazi.

"Mwanafunzi akipata alama tatu anakuwa amejihakikishia kupata ufadhili wa masomo, lakini kwa wanafunzi watakaoshindwa kuendelea kufanya vizuri katika masomo yao wanaondolewa kwenye ufadhili," alisema Prof. Anangisye.

Prof. Anangisye alisema mwaka juzi UDSM ilipokea wanafunzi 50 wa ufadhili wa masomo, hadi sasa wamebaki 35 huku wengine wakiwa wameondolewa kutokana na kushindwa kufanya vizuri katika masomo yao chuoni.

Alisema: "Utaratibu huu unafanywa na vyuo vingi duniani, sema sisi tumechelewa. Tunachokifanya leo siyo kitu kigeni."

## SUA yapata tawi la NMB

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

BENKI ya NMB imefungua tawi jipya mkoani Morogoro lililozinduliwa rasmi Jumatano katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Hatua hiyo ya kujidhatiti kibiashara pia inalenga kuimarisha uongozi wa benki hiyo katika utoaji wa huduma bora za kifedha.

Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara wa NMB, Filbert Mponzi, alisema tawi hilo limeleta ahuweni kwa wanajumuiya wa SUA na wananchi wanaoishi jirani na chuo hicho kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma za benki hiyo.

"Kabla ya tawi hili la NMB SUA, wateja wetu hususani wafanyakazi wa hapa SUA na wanafunzi walilazimika kusafiri hadi Tawi la NMB Wami lililopo katikati ya mji wa Morogoro zaidi ya kilometa sita kupata huduma za kibenki. Sasa wakazi wa Magadu, Mzinga, Kididimo, Misufini, Vibandani, Kasanga, Lugala na Mafiga huduma za kibenki tumewasogezea karibu," Mponzi alifafanua.

"Leo hii tunafungua tawi letu la NMB SUA, ambapo sasa wakazi wa Wilaya ya Morogoro watakua wamepata mahala pa kupata mahitaji yao yote ya kibenki," alifafanua na kuhamasisha matumizi endelevu ya tawi hilo.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Prof. Raphael Chibunda, aliwachagiza wana SUA, wananchi wanaoishi jirani na chuo hicho pamoja na wakazi wote wa Morogoro kuchangamkia fursa hiyo mpya kwa ajili ya maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla.

Alisema huduma za kibenki ni kati ya huduma muhimu sana kwa ustawi wa jamii na maendeleo ya kiuchumi na kuipongeza Benki ya NMB kwa kuwa mdau mkubwa wa maendeleo ya kiuchumi nchini.

Pia alisema sekta ya fedha ina umuhimu wa kipekee kimaendeleo kwani ndiyo inayowezesha shughuli zote za uchumi kama kuweka, malipo ya kibiashara na ya binafsi, uwekaji wa amana na kupatikana kwa mikopo ya aina zote.

Sambamba na uzinduzi huo, NMB imetoa msaada wenye thamani ya TZS milioni 16.2 wa vifaa vya hospitali, madawati kwa ajili ya shule ya sekondari ya chuo hicho na fedha kwa ajili ya mradi wa miti.

Meneja wa NMB Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper, aliliambia gazeti hili kuwa thamani ya mashine ya kufulia nguo za wagonjwa ni Sh. milioni 6.9 na viti vya kusukuma wagonjwa Sh. milioni 1.8.

BIASHARA

# TOSCI; chombo cha serikali kilicholeta mapinduzi mageuzi ya mbegu nchini

• Waleta mbegu 'feki'wanaangukia sheria; uagizaji mbegu nje umebakia 'kiduchu'



Huduma ya uandaaji mbegu ikiendelea katika maabara za TOSCI.

**Na Christina Haule,** MOROGORO

TAASISI ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu Tanzania - TOSCI) iliyo chini ya Wizara ya Kilimo ni siasa iliyoweka rekodi ya kuongeza matumizi ya mbegu bora zilizothibitishwa ubora kwa wakulima kutoka tani 10,946 (2014/2015) hadi tani 76,285 kwa mwaka 2019/2020.

Chombo hicho kwa jina rasmi 'Tanzania Official Seed Certification Institute' ambayo ndio imezaaa kifupi TOSCI, iko chini ya Wizara ya Kilimo na ilianzishwa kisheria mwaka 2003, kuchukua nafasi ya Wakala wa Taifa wa Kuthibiti Ubora wa Mbegu iliyoanzishwa mwaka 1973

TOSCI katika mfumo kuhudumia taifa, imejigawanya katika vituo vinne vya kanda na makao makuu yake ni mjini Morogoro, ikiwajibika na kusajili wafanyabiashara na wazalishaji mbegu, pia kufanya majaribio ya utambuzi na umahiri wa aina mpya za

> **Wote wanaokiuka miongozo ya sheria na kanuni za mbegu hufutiwa leseni walizonazo za biashara ya mbegu na kufunguliwa mashitaka mahakamani.**

mbegu (NPT).

Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI Patrick Ngwediagi, anasema wanatimiza majukumu hayo kwa kiwango cha asilimia 86.8, mbegu yote inayohitajiwa kitaifa inatoka nchini kupitia mikononi.

Anasema, hilo linafanyika, kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha upatikanaji, utumiaji na udhibiti ubora wa mbegu, ili kuongeza tija na kipato kwa wakulima, sambamba na usalama wa chakula na lishe.

Ngwediagi anasema, ni ongezeko linalotokana na ukuaji tasnia ya mbegu nchini na wizara kupitia TOSCI, imeongeza mbegu bora zilizothibitishwa nchini kutoka tani 4,337 katika mwaka wa fedha 2014/2015, hadi tani 64,304.7 za mwaka 2019/2020.

Katika hilo anasema, wametathmini jumla ya asilimia 84 ya mbegu zote zilizothibitishwa na mbegu bora kutoka nje ya nchi ni asilimia 16 pekee.

Ngwediagi, anazitaja sababu




Mbegu iliyoidhinishwa na TOSCI, tayari kwenda sokoni. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

zingine zilizochangia kuongezeka uzalishaji wa mbegu nchini ni pamoja na uwepo wa mazingira mazuri ya wawekezaji kwenye tasnia ya mbegu

Anasema kupanda matumizi hayo ya mbegu, ni matokeo ya juhudi za serikali kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji wa mbegu inayochangia kuongezeka uzalishia mbegu kutoka hekta 10,674 mwaka 2014/2015 hadi hekta 99,885 mwaka 2019/2020.

Anasema, Wizara ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo (TARI) na kampuni za mbegu, zimeimarisha utafiti wa aina mpya za mbegu na kuwezesha kupatikana zile zinazotoa mavuno mengi, kuhimili ukame, magonjwa na wadudu.

Pia, anasema Wizara ya Kilimo kupitia TOSCI, imeimarisha majaribio ya utambuzi na umahiri wa aina mpya za mbegu, hivyo inahakikisha kuwapo aina zote za mbegu zinazodhibitishwa na TOSCI zinakuwa na vigezo vyote muhimu kabla hazijasajiliwa.

Kutokana na juhudi hizo za kiserikali, aina mpya za mbegu zilizosajiliwa zimeongezeka kutoka aina 431 (2015/2016) hadi aina 604 (2019/2020).

Hata hivyo, Mkurugenzi Mkuu wa TOSCI anasema kuongezeka matumizi ya mbegu bora, imepunguza changamoto ya mbegu feki inayotishia ustawi wa tasnia ya mbegu nchini.

Katika kukabiliana nma hali hiyo, Ngwediagi anasema TOSCI ilichukua hatua zilizoonyesha matokeo chanya, kwa kupunguza matukio ya mbegu feki kutoka matukio 327 mwaka 2014/15 hadi matukio matano kwa mwaka wa kilimo 2019/20.

Anasema, TOSCI imeshafanikiwa kupunguza matukio ya mbegu feki, baada ya kuhakikisha kunakuwapo udhibiti wa ubora wa mbegu, ambao wizara kupitia TOSCI, imeweka utaratibu wa kuongeza matumizi ya nembo za ubora za TOSCI katika kila mbegu iliokaguliwa.

Mkurugenzi huyo anasema, katika mwaka wa fedha 2019/20 jumla ya nembo 9,000,000 zimetolewa na wakala huyo wa kiserikali wa mbegu kwa wazalishaji, ikilinganishwa na nembo 400 za miaka mitano kabla, 2014/15.

### KUKABILI UTAPELI

Hata hivyo, Ngwediagi anasema ili kuhakikisha wafanyabiashara ya mbegu wasio waaminifu hawaingizi sokoni mbegu feki, TOSCI na mdau wake kampuni ya simu TTCL, zimebuni mfumo wa kielektroniki utakaowawezesha wakulima kubaini mbegu feki, zilizo na nembo feki.

Hiyo inatajwa inatokana na kupungua kiasi kikubwa, au hata kuwapo matukio ya wauza mbegu feki au zisizo na viwango, huku akitaja mafanikio yaliyopo ni watu wengi sasa wanapendelea kununua mbegu zenye nembo ya TOSCI.

Ngwediagi anasifu hatua ya kutoa elimu kwa umma kumesaidia kupunguza matukio ya mbegu feki, hasa zikipitia kwa watoa elimu kwa wakulima na umma juu ya utambuzi wa mbegu feki kwa kupitia magazeti, radioni, runinga, semina, warsha na mikutano.

Ngwediagi anasema, TOSCI imekuwa ikifanya ukaguzi wa maghala na maduka yanayouza mbegu mara kwa mara hasa wakati wa msimu wa kilimo ambapo imepanua wigo wa ukaguzi wa maduka yanayouza pembejeo mbegu ili kuhakikisha kuwa wauzaji wote wa mbegu wanafuata sheria na kanuni za mbegu hivyo kuuza mbegu zilizo na ubora unaotakiwa.

Aidha anasema pia wamekuwa na utaratibu wa Kuhakikisha kuwa wafanyabiashara ya mbegu wote wanasajiliwa kabla ya kuanza biashara ili kuwafanya waweze kufuata sheria na kuzijua kanuni za mbegu.

Anasema tangu TOSCI imepewa jukumu la kusajili wauzaji wa mbegu baada ya mabadiliko ya sheria ya mbegu ya mwaka 2014, ambayo taasisi inahakikisha wauza mbegu wanakidhi vigezo vya TOSCI, ikiwamo; kupata mafunzo ya mbegu, sheria na kanuni, kuwa na leseni ya biashara na nambari ya mlipa kodi - TIN.

Hivyo Ngwediagi anasema baada ya kukidhi vigezo hivyo mfanyabiashara wa mbegu hupewa cheti cha usajili cha TOSCI, hivyo kuwa na haki ya kuuza mbegu. Lengo ni kuhakikisha wazalishaji wa mbegu nchini wanasajiliwa na wanafuata sheria na kanuni za mbegu.

Anasema, wote wanaokiuka miongozo ya sheria na kanuni za mbegu hufutiwa leseni walizonazo za biashara ya mbegu na kufunguliwa mashitaka mahakamani.

Mkurugenzi Mkuu anasema, kutokana na kuwapo changamoto ya wakaguzi wachache wa mbegu, anawataka wakulima wawatumie vyema, kwa sababu taasisi iliandaa mpango mkakati wa miaka mitano unaoishia mwakani.

Hiyo iliendana na mafunzo kwa maofisa kilimo wilaya na waliowasajili wasaidie kusimamia ubora wa mbegu kwa niaba ya TOSCI. Hadi sasa wamekwishawaidhinisha wakaguzi 160 kati ya 400 wanaohitajika.

Ngwediagi anasema, wanaendelea kuimarisha uthibiti wa ubora wa mbegu zinazoingizwa kutoka nje ya nchi huku lengo ni kuhakikisha mbegu zote kutoka nje ya nchi zinapewa vibali na TOSCI na kuhakikisha zinafuatiliwa kuona kama zimekidhi vigezo vya ubora vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria ya mbegu.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Tuikabili nimonia kama ilivyokuwa mwaka jana





**NA JOSEPH KULANGWA**
**(+255) 713 410008**
**jkulangwa@yahoo.com**

DUNIA inapitia kipindi kigumu sana kutokana na maradhi haya mapya yaliyoikumba, Tanzania ikiwa ni sehemu yake na ambayo inapambana kuhakikisha nayo inanusurika.

Hivi sasa kila eneo duniani gumzo na harakati ni kuhusu Uviko-19, maradhi ambayo yaliibuka mwaka jana yakiaminika kutokea China na kusambaa duniani kote, yakiua idadi kubwa ya watu.

Uviko unaenezwa kwa hewa maji, maambukizi yake yanakuwa ya haraka sana sambamba na vifo vyake, huku watu wakitakiwa kujihami kwa kudumisha usafi, pia kujiepusha na mikusanyiko.

Miito mbalimbali ilitolewa mwaka jana, huku wataalamu walijitahidi kutafuta chanjo ya kinga ya maambukizi ya ugonjwa huo, ambayo hivi sasa zimeanza kusikika katika mataifa mbalimbali duniani na hata majaribio yameanza.

Watanzania baada ya kupoteza watu mwaka jana, tuliendelea kupokea maelekezo ya kitaalamu kutoka kwa wataalamu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee an Watoto, wakitutaka kujihadhari kwa kunawa mikono kwa majitiririka na sabuni.

Pia, tukitakiwa kuvaa barakoa tuwapo kwenye mikusanyiko na kujiepusha na misongamano, kutakasa mikono kwa vitakatishia ambavyo vimekuwa vikipatikana katika maduka mbalimbali ya dawa za binadamu.

Lakini, kubwa likawa ni mwito wa Rais kuwataka wananchi kufungana kumwomba Mungu. Ni mwito uliosikilizwa na wananchi na baadaye kuaminika, kuwa Mungu alisikia na kuondoa janga la Uviko.

Wananchi waliacha kuvaa barakoa, kunawa, kujitakasa na kurudia mikusanyiko kama kawaida, huku tukikataa kabisa kujifungia ndani, kwa kuchelea kuathirika kiuchumi.

Baada ya kuamini kwamba Uviko umetoweka, tulijiachia kana kwamba hakukuwahi kuwa na janga hilo nchini, huku mataifa ya nje yakiendelea kulia, kuzikana kutafuta mbinu za kukabiliana na ugonjwa huo, watu wao wakichukua hadhari za kitaalamu.

Hivi sasa wakati mataifa ya nje yakisema virusi vya corona sasa vimekuja kwa sura nyingine, huku kwetu inaelezwa kuna namna ya madhara yaliyoanzia upande wa Kusini mwa Afrika.

Tunasikia nchi kuingia 'Nimonia' na 'Changamoto ya Kupumua' ambayo kwa kweli vinatudhuru.

Dalili za Uviko na Nimonia, kwa kweli zinaangukia kapu moja, madhara yanafanana na maambukizi kwa staili ileile. Ni kama magonjwa pacha. Hivyo, ni vema tujikinge kama tulivyopata kufanya mwaka jana wakati wa Uviko.

Kasi ya mwitikio ya nini cha kufanya sasa, nadhani haijafikia ile ya mwaka jana. Inawezekana nguvu ya hamasa ya sasa, haifikii ile ya mwaka jana.

Kwa kuwa Uviko na Nimonia ni kama mtu na mdogo wake, inafaa kasi ya msukumo iongezeke na mwamko uwe maradufu ya sasa.

Kinyume chake, huenda kila mmoja atajifukiza kwa kasi ndogo na kwa namna utashi na uelewa wake uliko, vivyo hivyo katika matumizi ya dawa, wengine wanaopotoka uelewa wanameza wajuacho au kuamini.

Hiyo inaangukia katika athari, hata kuwapo wanaotumia dawa wataalamu wanazitambua ni za matende, wakiamini zinatibu nimonia! Alamsiki!

UCHUMI

KAMANDA KIBWENGO:

# TAKUKURU Dodoma inalia na miradi, ufuatiliaji na darasa 'mguu kwa mguu'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMANDA wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Dodoma, Sosothenes Kibwengo, anaitaja miradi ya maendeleo ni muhimu kwa taifa, kwa sababu inainua uchumi wa nchi na jamii kwa jumla.

Anasema, kutokana na hali hiyo huwa wanatumia kila mara mustakabali huo katika harakati za kupambana na rushwa jijini, kwani inaugusa mkoa na ustawi wa wananchi kwa jumla, ikizingatia taifa liko katika uchumi wa kati.

Kibwengo anasema TAKUKURU mpakani humo imekuwa ikifuatilia kwa karibu kuhakikisha utekelezwaji wake, kuwanufaisha wananchi kiuchumi na jijini Dodoma imeshafuatilia jumla ya miradi 43 yenye thamani ya Sh. bilioni 19.6 katika sekta za Maji, Afya, Elimu, Biashara, Fedha na Ujenzi.

Anasema asilimia kubwa ya miradi hiyo ilionekana kutekelezwa kwa kuzuingatia kanuni na taratibu husika, wakati huo huo, ikitoa elimu kwa wananchi waliopo katika maeneo iliko miradi, umuhimu wa kuifuatilia na kuitambua ili kuwasaidia kimaendeleo wao na familia zao.

Kwa mujibu wa Kamanda Kibwengo, maelekezo ya kurekebisha miradi iliyobainika kuwa na mapungufu yalitolewa na kuna sehemu zilifanyika warsha, wadau walijadili upungufu na mianya ya rushwa, hata wakaweka maazimio ya kuirekebisha, ili thamani ya fedha iliyotolewa ionekane.

Kibwengo anaeleza TAKUKURU inatoa elimu kwa wasimamizi miradi na kamati za ununuzi vifaa miradi, ili waendane na sheria, pia taratibu za nchi, uamuzi ukifanywa na vikao halali, kumbukumbu za kila uamuzi na ununuzi kuhifadhiwa, ili kujiepusha na rushwa. Anasema walipofuatiliaji, kuna miradi mitatu ilionekana kuwa na viashiria vikubwa vya jinai na uchunguzi dhidi yake inaendelea kutekeleza.

Kibwengo anasema, TAKUKURU mkoani Dodoma, kwa kipindi kuanzia Julai mwaka jana hadi sasa wamefanikiwa kutekeleza mambo mengi kulingana na mpango mkakati wa TAKUKURU, wakizingatia maelekezo ya Rais Dk. John Magufuli.

Anasema wanazingatia vipengele vinne wakati wa ufuatiliaji miradi ya maendeleo, akianza na kukagua ucheleweshaji mradi unaotokana na uzembe au vitendo vya rushwa, katika utoaji fedha zilizoidhinishwa na serikali kwa ajili ya mradi husika.



Mkuu wa TAKUKURU mkoani Dodoma, Sosthenes Kibwengo, akimkabidhi fedha Mwalimu Mstaafu Juma Bura zilizorejeshwa na kampuni iliyodaiwa kumpatia 'mkopo umiza' **PICHA: RENATAHA MSUNGU.**

> **Kutokana na utekelezaji uliopo, taasisi imewezesha kunusuru haki ya nyumba moja, viwanja 21 na mashamba mawili yenye jumla ya ekari 15.**

Pia, anasema kuna uchepushaji wa fedha na rasilimali nyingine za miradi kwenda kwenye sekta au watu binafsi bila kuzingatia taratibu za nchi na wanaangalia, iwapo kuna ushirikishwaji wa kutosha wa wananchi wa eneo husika, jambo ambalo ni muhimu kupanua wigo wa wasimamizi.

Mwisho, anataja wanasimamia kuona kama mradi husika una thamani halisi ya kifedha.

#### TAARIFA DODOMA

TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, zinaonyesha kwamba, walifuatilia miradi ya maji ya vijiji vya Kelema Kuu na Mlongia wilayani Chemba, pamoja na makandarasi husika kurejesha fedha walizolipwa kinyume na taratibu.

Pia, walirekebisha miradi hiyo na ikaanza kutoa maji, jambo lenye maslahi mapana kwa wananchi wa maeneo hayo na serikali kwa ujumla.

"Hii imesaidia sana wakazi wa maeneo hayo, hivi sasa hufanya vitu mbalimbali vya kujikwamua kiuchumi kupitia maji wanayopata," anasema Kibwengo.

Anatoa wito wananchi wa Mkoa wa Dodoma, kuthamini miradi iliyo katika maeneo yao, kuifuatilia na kushirikiana kuisimamia, kwani ni miradi yao inayotekelezwa kwa fedha zao na ndio wanufaika wakubwa, hivyo hawana budi kuwa waangalizi wanapoona kuna vitendo vya rushwa.

Kibwengo anasisitiza kuona miradi hiyo inafanyiwa ubadhirifu na wananchi wananyamaza bila ya kukemea wala kutoa taarifa kwa TAKUKURU au mamlaka nyinginezo za serikali, ni sawa na kushiriki uovu huo.

#### UCHAMBUZI MIFUMO MAENEO

Kamanda Kibwengo anasema, kuanzia Julai, 2020 kwa kutumia Ofisi ya Mkoa na wilaya za Kondoa, Kongwa, Chemba, Mpwapwa, Bahi na Chamwino, wamefanya uchambuzi wa mifumo ya utendaji na uhitaji huduma 24 na kubaini mambo mbalimbali yanayowezesha kuwapo vitendo vya rushwa.

Kibwengo anasema, mifumo hiyo ni katika sekta za Kodi, Utawala, Maji, Afya, Mikopo na Ujenzi na ziliwashirikisha wadau na matokeo ya uchambuzi yalijadiliwa na kuwekewa maazimio ya utekelezaji na hadi sasa, tayari taarifa sita za utekelezaji wa maazimio zimeshapokelewa.

Uchambuzi wa mianya ya rushwa katika mfumo wa ukusanyaji ushuru, wahudumu ulifanyika katika wilaya zote za Mkoa wa Dodoma, ambako mambo yanayochangia kuzorota ukusanyaji wa ushuru huo yalibainishwa na maazimio ya kuboresha utolewaji.

Anasema, ufuatiliaji wa matokeo hayo umeonyesha kwamba baadhi ya makandarasi wanaofanya miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara, hawalipi kodi hiyo kwa halmashauri zetu.

#### TAKUKURU VS WADAU

Ushirikiano kati ya TAKUKURU Dodoma, Mamlaka ya Majisafi na mazingira Dodoma (DUWASA) na Halmashauri ya Jiji Dodoma, umewezesha wadau kushirikiana kuwaelimisha na kuwabana kimkataba makandarasi kulipa kodi wanaodaiwa.

Inaelezwa kwamba, kunatarajiwa makandarasi wanaosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Kibwengo anajisifu kuwa utekelezaji wa jukumu la kuzuia rushwa na kazi ya kuimarisha utawala bora umeifanya TAKUKURU Dodoma kuokoa au kudhibiti jumla ya Sh. bilioni 1.9 (1,908,130,411), fedha za miradi ama zilizofujwa au kuchepushwa.

Malipo yaliyofanyika kinyume na taratibu, madeni sugu ya vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS), Mfuko wa Pembejeo, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na 'mikopo umiza.'

Anaongeza, kutokana na utekelezaji uliopo, taasisi imewezesha kunusuru haki ya nyumba moja, viwanja 21 na mashamba mawili yenye jumla ya ekari 15.

Ni jambo ambalo Kibwengo anaeleza, limewezesha baadhi ya miradi ya maendeleo ambayo yalikwama kukamilika na kuwezesha wananchi kufaidi matunda ya juhudi za serikali yao.

Kibwengo anaitaja 'mikopo umiza' ambayo kimsingi ni ile ya masharti magumu, riba kubwa na inachukua muda mrefu, ambayo ilirejeshwa kwa wananchi wanyonge na kuwawezesha kupata matumaini ya kuendeleza biashara kwa uhuru sasa.

# Wanaopeleka matunda Dodoma wapewa angalizo

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

UMOJA wa Masoko Rasmi Jiji la Dodoma (UMADO), umewataka wafanyabiashara wanaopeleka matunda, mboga na viazi kutoka nje ya mkoa, kuheshimu na kutekeleza maelekezo yanayotolewa na Halmashauri ya Jiji ikiwamo kushusha mizigo kwenye Soko la Job Ndugai.

Rai hiyo ilitolewa jana na viongozi wa umoja huo jijini hapa walipokuwa wakitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari kuhusu agizo la Halmashauri ya Jiji kwa wafanyabishara wote wanaoleta mizigo yao kwa kutumia magari kushusha kwenye Soko la Job Ndugai na siyo eneo lingine.

Makamu Mwenyekiti wa umoja huo, Goha Magwai, alisema kinachotakiwa ni kutii maelekezo hayo ambayo yaliyotolewa na halmashauri ili kufanya kazi kwa uhuru na ufanisi.

Alisema wafanyabiashara ambao wanaleta biashara hizo, hakuna sababu ya kuvutana na maelekezo hayo na halmashauri kuhusu katazo hilo, bali watoe mapendekezo namna ya kuboresha utendaji badala ya kuvutana.

Alisema serikali imewekeza mabilioni ya shilingi katika Soko la Ndugai kwa ajili ya wafanyabishara wadogo na wakubwa, hivyo wanatakiwa kutoa ushirikiano ili kutatua vikwazo vilivyomo ndani ya soko hilo.

Marwa Mabucha, Mwenyekiti wa umoja huo, aliomba halmashauri hiyo kufanya maboresho kwenye eneo wanalotakiwa kushusha mizigo yao ili kuondoa tofauti iliyopo sasa.

Alisema maboresho hayo yanajumuisha halmashauri kutenga eneo ambalo wafanyabiashara wanaoleta biashara kutoka nje ya mkoa, wapewe sehemu ya kufanyia biashara badala kusafirisha hadi kwenye masoko mengine.

"Tunaiomba halmashauri yetu hii ya jiji, kutuboreshea eneo hili tunaloshushia mizigo, ili tuweze pia kuuza biashara baada ya kushusha mizigo badala ya kupeleka yote kwenye masoko mengine," alisema.

Fortunatus Keela, mfanyabiashara wa soko la matunda na mboga la Bonanza, aliishauri halmashauri kukaa pamoja na wafanyabishara ili kutatua vikwazo vinavyotokea kwa maendeleo ya jiji na mustabakabili mpana wa Sekta ya Biashara.

Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, akizungumza na wafanyabiashara kwa nyakati tofauti ambao wanaleta bidhaa hizo kwa kutumia magari, aliwataka kufuata maelekezo.

Alisema serikali imewekeza mabilioni ya fedha kwa ajili ya wafanyabiashara kulitumia soko hilo la Ndugai, hivyo kama kuna kasoro, wanatakiwa kukaa kwa pamoja ili kuzitatua.

"Badala ya kuvutana kati yao na halmashauri badala yake watumie vikao ambavyo vinaleta majibu ya haraka kufurahia soko hilo tofauti na ilivyo kwa sasa," alisema.




Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri (katikati), akizungumza na Meneja wa benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi (kulia) na Meneja Uhusiano na Serikali wa benki hiyo, Kanda ya Kati, Peter Masawe, walipomtembelea ofisini kwake juzi. **PICHA: IBRAHIM** JOSEPH

# TALIRI yawapa mbinu wafugaji kuku

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KAIMU Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Mpwapwa, Aluna Chawala, amewataka wafugaji wa kuku kuzingatia ushauri unaotolewa na watafiti wa mifugo, ili wafuge kisasa na kuinuka kiuchumi.

Chawala ametoa ushauri huo ikiwa ni siku chache baada ya Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi kukutana na wafugaji kuku na kubainisha mifugo hiyo sasa itauzwa kwa kupimwa katika mizani badala kukadiria.

Alisema hivi sasa wafugaji wanapaswa kufuga kisasa kutokana na mifugo hiyo kuanza kuuzwa kwa kupima kwa kilo katika mizani badala ya kukadiria, uamuzi ambao anaamini utasaidia kupata faida. "Ninaomba wafugaji wa kuku waanze kufuga kisasa ili waendane na soko la kisasa ambalo litawasaidia kuinuka kiuchumi," alisema Chawala.

Pia, alisema kuku anapofugwa kisasa kwa kupata matunzo mazuri kutoka kwa mfugaji, lazima atakuwa na uzito mkubwa ambao utasaidia kuuzwa kwa bei nzuri sokoni.

"Tunahitaji kuona wafugaji wanainuka kiuchumi kupitia biashara wanayofanya hasa ukizingatia taifa liko katika uchumi wa kati," alisema Chawala.

Aliwataka wafugaji kuzingatia elimu ya ufugaji kuku kisasa inayotolewa na watafiti mbalimbali, ili kuhakikisha wanafuga kisasa na kupata kipato kikubwa ambacho kitawasaidia wao na familia zao.

Alisema ifike wafugaji wabadilike na kuanza kufuga kisasa kwa kutumia kanuni ambazo zimefanyiwa utafiti ili wafanye biashara yenye tija.

Vilevile, alisema kuuza kuku kwa makadirio kwa wafugaji wanavyofanya katika biashara hiyo, inafanya kipato chao kinakuwa kigumu kwa sababu wanauza kwa bei ya hasara.

Alisema umefika wakati sasa wafanyabiashara na wafugaji wabadilike na kufanya shughuli zao kisasa ili kupiga hatua kwa kuingia katika soko la kimataifa la uuzaji kuku wa nyama.

# Ufuatiliaji miradi ya maji waleta matokeo chanya

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MRADI wa kujenga uwezo kwa jamii na asasi za kiraia katika ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma kwenye miradi ya maji, umetajwa kuleta matokeo chanya kwa wananchi kushiriki kulinda na kufanya miradi kuwa endelevu.

Hayo yalibainishwa jana jijini hapa ilipowasilishwa taarifa za mradi huo unaotekelezwa na Mtandao wa Asasi za Kiraia Mkoa wa Dodoma (NGONEDO) kwa ufadhili wa Foundation for Civil Society (FCS).

Akizungumza kwenye mkutano huo, mwakilishi kutoka Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), Samson Njoweke, alisema kabla ya mradi huo kutekelezwa, wananchi walikuwa wakiona miradi hiyo ni mali ya serikali.

Alisema kutokana na mradi huo, hivi sasa wananchi wamepata uelewa na kuona miradi ya maji ni mali yao na wanatakiwa kuitunza ili iwe endelevu.

Njoweke alisema kisera, bado kuna upungufu kutokana na baadhi ya mifumo kubadilika na wananchi hawajahusishwa kikamilifu.

Alisema serikali inafanya kazi zake kikamilifu kwa kushirikiana na wadau katika kutatua vikwazo katika upatikanaji maji wilayani Bahi mkoani Dodoma.

Alisema wananchi wamekuwa wakichukua hatua mbalimbali kwa kuwa uwazi na ufuatiliaji wa miradi umekuwa mzuri. "Mimi ni mratibu wa vyombo vya watumiaji maji Wilaya ya Bahi. Hata mimi zamani wenyeviti wa vijiji nilikuwa ninawaona kama maadui, lakini nilipogundua ushirikishwaji ni muhimu kwenye miradi ya maji, sasa wananchi wamekuwa walinzi namba moja wa miundombinu ya maji," alisema.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mchito, Abdul Machete, alisema kamati za PETS zinafanya kazi vizuri kwa kuwa zimepewa uwezo na kila siku zinaongeza uelewa katika utendaji.

Mjumbe wa kamati za PETS, Hussein Mwaja, alisema kamati zimewapa uelewa na hivi sasa wanaona miradi ya maji ni mali yao na siyo serikali.

Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Honoratha Rwegasira, alitaka matokeo chanya yaliyopatikana kutokana na utekelezwaji wa mradi huo katika Wilaya ya Bahi yaendelezwe ili jamii iendelee kufaidika na fursa za uwapo wa miradi ya maji.

Akitoa tathimini ya utekelezaji wa mradi huo, Luhaga Makunja kutoka NGONEDO, alisema Wilaya ya Bahi ina vijiji 59, lakini mradi huo ulitekelezwa katika vijiji vinne tu ambavyo ni Mkakatika, Bahi Sokoni, Nguji na Mkito.

Alisema sasa wananchi asilimia 70 wana uelewa wa miradi ya maji na ufuatiliaji wa miradi ya maji umeongezeka.

Alisema wakati wa utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi, ziliundwa kamati za kufuatilia matumizi ya fedha za umma (PETS) za vijiji na kulikuwa na mafunzo baadaye awamu ya pili ilitoa mafunzo ya ufuatiliaji ikiwamo ufuatiliaji wa nyaraka.

Alibainisha kuwa hadi kufikia mwaka 2020, Bahi ilikuwa na asilimia 50 ya wananchi wanaopata maji.



# Mtayarishaji nyimbo za injili matatani tuhuma kukutwa na bunduki, risasi

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linamshikilia mtayarishaji wa nyimbo (Producer), Joseph Mwamakusi (30), Mkazi wa Iyela kwa tuhuma za kumiliki silaha.

Inadaiwa kuwa mtuhumiwa huyo alikutwa na bunduki aina ya Shortgun iliyokatwa mtutu na kitako yenye namba za usajili 5481 na risasi zake 11 na Bastola 01 aina ya Bereta iliyofutwa namba za usajili ikiwa na risasi moja ndani ya magazine bila kuwa na kibali.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, kwa vyombo vya habari jana, mtuhumiwa alikamatwa juzi majira ya saa 3:30 asubuhi.

Alisema taarifa hizo walizipata kutoka kwa msamaria mwema na kwamba silaha hizo zilikutwa ndani ya mfuko wa sandarusi kisha kuwekwa kwenye begi dogo ndani ya nyumba yake.

Kamanda Matei alisema hadi sasa, mtuhumiwa ametiwa nguvuni na kwamba uchunguzi bado unaendelea kubaini ukweli wa suala hilo na ukikamilika, atafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zinazomkabili.

Alitoa wito kwa wananchi kuacha tabia ya kumiliki silaha za moto kinyume cha taratibu kwa kuwa zinahatarisha usalama wa wananchi.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mbeya walilishauri Jeshi la Polisi kuangalia upya utoaji wa vibali vya kumiliki silaha za moto kwa watu binafsi kwa madai kuwa baadhi huzitumia vibaya na kuhatarisha usalama.

Miongoni mwao, ni Jerome Ambakisye, mkazi wa Forest, aliysema baadhi ya wananchi wanaopewa vibali vya kumiliki silaha, huzitumia kutishia watu pindi wanapopishana kauli na kulishauri Jeshi la Polisi kuangalia upya utoaji wa vibali.



Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, akizungumza na wananchi wa Kata ya Mwansekwa, jijini Mbeya jana, kuhusu umuhimu wa upimaji ardhi ambao unatarajiwa kuanza hivi karibuni. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Halmashauri yapata dawa ujenzi holela

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya imeanza mikakati ya kupima ardhi katika Kata ya Mwansekwa ikiwa ni utekelezaji wa mpango kabambe wa jiji hilo ambao ulibuniwa hivi karibuni kukabiliana na ujenzi holela wa makazi.

Mkakati huo ulianza kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu faida ya upimaji wa ardhi pamoja na mpango kabambe wa jiji hilo ambao umeanza kutekelezwa.

Akiwasilisha mpango kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika kata hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Jiji la Mbeya, Amede Ng'wanidako, alisema mabadiliko ni lazima yafanyike kwa sababu mji unakua kwa kasi.

Mkurugenzi huyo alisema mbali na kutaka kuupanga vizuri mji huo, upimaji wa ardhi ya wananchi pia unasaidia kuiongeza thamani kwa maelezo kuwa uwanja uliopimwa, bei yake ni tofauti na ile isiyopimwa.

"Halmashauri ya Jiji la Mbeya imekuja na mkakati wa kupima ardhi katika maeneo mbalimbali. Leo (jana) tupo Kata ya Mwansekwa kwa ajili ya zoezi hili na tutapima maeneo yote yaliyo kwenye mkakati.

Kabla ya kufanya hivyo, tutatoa elimu kwa wananchi kutambua umuhimu wa zoezi hilo," alisema.

Ngw'anidako alisema wananchi wote lazima washirikishwe kwenye mchakato huo kuanzia hatua za awali hadi kwenye zoezi la upimaji ardhi, ili kutambua malengo ya serikali kutekeleza katika eneo hilo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, aliwatoa hofu wananchi wa Mwansekwa na kuwaahidi kuwa kila mwenye ardhi atapatiwa haki yake.

Alisema upimaji ardhi utatoa kipaumbele kwa wamiliki wa ardhi wa asili kwa kuhakikisha kila mmoja anapata stahiki zake huku akiutaka uongozi wa kata kutoa elimu zaidi juu ya umuhimu wa upimaji ardhi.

## DC ashtuka ufaulu duni wa sekondari

**Na Mwandishi Wetu,** MBARALI

MKUU wa Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Reuben Mfune, amewataka wenyeviti wa bodi za shule za sekondari, waratibu elimu na wakuu wa shule hizo, kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuongeza ufaulu.

Mfune alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kikao cha kujadili namna bora ya kuongeza ufaulu kwa shule za sekondari wilayani humo.

Alisema licha ya serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu, kikwazo kipo kwa watumishi katika kuongeza ufaulu.

Alisema kikao hicho kilijadili mikakati ya namna ya kuongeza ufaulu kwa kutumia mbinu shirikishi baina ya wanafunzi na walimu kwa kushirikiana na wazazi.

"Tumekaa kikao kazi cha kujadili namna bora kuongeza ufaulu. Miongoni mwa mbinu tunazoona zinafaa, ni kuanzisha utaratibu wa wanafunzi kula chakula shuleni, watoto kukaa hosteli na kuanza utaratibu wa masomo ya jioni," alisema Mfune.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Kivuma Msangi, alisema walimu wote watakaokuwa wanafaulisha wanafunzi kwenye masomo wanayofundisha ufaulu wa daraja A na B watakuwa wanapatiwa zawadi kama motisha na ofisi yake.

Alisema licha ya baadhi ya shule za sekondari kutokufanya vizuri, serikali inaendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya elimu, akibainisha kuwapo sekondari 32 zikiwamo nne mahususi kwa wasichana.

Mkuu wa Idara ya Elimu ya Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Anna Shitindi, alisema wamejipanga kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wote wa shule za sekondari kwa kuhakikisha wanaandaa mitihani ya awali kabla ya mitihani ya taifa.

Alisema wataendelea kuhamasisha wazazi kuchangia chakula shuleni pamoja na kufanya ufuatiliaji wa mara kwa mara kwa shule zote kubaini dosari zinazojitokeza.





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizungumza na kuwapongeza madaktari bingwa wazalendo wa kitengo cha upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, katika hafla iliyofanyika Ikulu, jijini Zanzibar juzi. **PICHA: IKULU**

# Mchango wa vyombo vya habari watajwa

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

VYOMBO vya habari vimetajwa kuwa vina mchango mkubwa katika kutunza na kuhamasisha amani na ustawi wa wanajamii katika nchi.

Hayo yalielezwa na Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Kaskazini "A", Khatibu Abibu Ali, wakati akifungua warsha ya siku moja ya waandishi wa habari wa wilaya hiyo yaliyolenga umuhimu wa vyombo vya habari katika utatuzi wa migogoro katika jamii.

Alisema jamii zimekuwa na utamaduni wa kufuatilia vyombo vya habari pamoja na kuamini taarifa zote zinazotolewa na vyombo hivyo kuwa ni sahihi hususani katika vipindi vya uchaguzi au yanapotokea maafa.

Alisema endapo waandishi wa habari au chombo cha habari kikakosea kutoa taarifa, hali hiyo huleta athari kwa jamii na hata muda mwingine jamii hushuku mamlaka husika kwa kudhani inaficha ukweli kutokana na taarifa isiyosahihi waliyoisikia katika vyombo vya habari. Aidha, akitolea mfano katika Kisiwa cha Tumbatu ambapo alisema vyombo vya habari ndio vimechangia kurejesha amani katika kisiwa hicho baada ya kuathiriwa na mivutano ya kisiasa ya muda mrefu husasani katika vipindi vya uchaguzi.

Alisema serikali ilishirikiana na waandishi wa habari pamoja na radio jamii kufanya vipindi vingi vya umuhimu wa amani pamoja na athari za kutoweka amani pamoja na kufanya mijadala iliyowakutanisha watu wenye itikadi mbalimbali za vyama na hatimaye lilifanikiwa.

"Asilimia kubwa nchi ambazo huingia katika machafuko huanzia katika vyombo vya habari tumeona mfano wa Rwanda, vyombo vya habari vinaweza kuleta amani katika nchi au vinaweza kuivuruga ndani ya saa chache tu, hivyo tunaomba mwendelee kuhubiri amani maana athari za machafuko zinajulikana na nchi inayoingia katika machafuko kurejesha amani iliyotoweka ni mchakato wa muda mrefu sana," alisema.

Akiwasilisha mada, mwezeshaji wa warsha hiyo, DK. Mohmed Hafidh Khalfani, alisema waandishi wa habari wamechangia katika kuituliza jamii katika kipindi cha kabla na hata baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Alisema licha ya wanasiasa nao kuwa mstari wa mbele katika kuangalia zaidi maslahi ya wananchi kwa kuangalia athari za migogoro, lakini waandishi wa habari hawakuwa vichocheo pengine vya jamii kufanya fujo.

Aliwataka waandishi wa habari kuhakikisha wanaendelea kuhubiri amani katika jamii sehemu zote ambazo wanahisi kuna migogoro na pengine migogoro hiyo inaweza kuleta vurugu na mivutano.

Kwa upande wake Mratibu wa Jumuiya ya Jukwaa la Vijana Zanzibar (ZYF), Almasi Mohmed Ali, alisema lengo la mradi huo umelenga kuleta mshikamano katika jamii ili kuepusha migogoro ya aina mbalimbali.

Alisema vyombo vya habari vinachangia katika kuleta mshikamano katika jamii na kuepusha mivutano kwa kufanya vipindi mbalimbali vinavyoelezea umuhimu wa amani katika nchi.

Warsha hiyo ya siku moja ilifanyika huko katika Shule ya Mkwajuni Mkoa wa Kaskazini Unguja na kuandaliwa na ZYF chini ya mradi wa Kukuza Umoja wa Kitaifa unaotekelezwa katika wilaya tatu za Unguja na wilaya moja kisiwani Pemba.

## Sababu idadi ndogo wanawake wenye ulemavu katika siasa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

USHIRIKISHWAJI mdogo wa wanawake wenye ulemavu katika vyama vya siasa, umechangia kupatikana kwa asilimia ndogo ya wanawake wenye ulemavu kushiriki katika nafasi za uongozi.

Hayo yalielezwa na Ofisa Mfuatiliaji Tathmini na Mafunzo wa Jumuiya ya Wanawake wenye ulemavu Zanziar (JUWAUZA), Mujuni Baitan, wakati akiwasilisha tathmini ya mchakato wa uchaguzi wa mwaka 2020.

Alisema baada ya kumalizika kwa uchaguzi mkuu, jumuiya yao ilifanya tathmini na kubaini kuwa wanawake wenye ulemavu walipata nafasi za uwakilishi ni asilimia 24.3 ambayo ni ndogo ukilinganisha na idadi ya vyama vya siasa vilivyopo.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo, jumuiya yao imeandaa mikakati maalumu ambayo itawawezesha wanawake wenye ulemavu kutatua changamoto zinazo wakabili katika uchaguzi.

Naye Katibu wa Jumuiya hiyo, Mwandawa Khamis Mohammed, alisema wameanzisha mradi maalumu wa kuwahamasisha wananchi wa vijijini juu ya kujuwa umuhimu wa kuwa na vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wao.

Alisema mradi huo umekuwa ukitoa elimu kwa watu wenye ulemavu juu ya watoto wenye ulemavu kutokana na watoto wengi wenye ulemavu kukosa vyeti vya kuzaliwa.

Washiriki wa mkutano huo ambao uliwashirikisha waandishi wa habari, waliiomba jumuiya hiyo, kuendelea kuwaelimisha watu wenye ulemavu juu ya umuhimu wa kushiriki katika masuala mbalimbali ya kijamii.

# Mwinyi aona dalili Zanzibar kutoa huduma za kibingwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema ndoto yake ya kuifanya Zanzibar iwe sehemu ya kutoa tiba za kibingwa sasa imeanza kutimia.

Dk. Mwinyi alisema hayo wakati akiwapongeza madaktari wa Hospitali ya Mnazimmoja baada ya kufanya upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo na mishipa ya fahamu katika Hospitali ya Mnazimmoja ambao aliwaita Ikulu kwa lengo la kuwapongeza.

Pongezi hizo zimekuja baada ya kitengo hicho cha wataalamu kumfanyia upasuaji mgonjwa, Keleshi Belinda, raia wa Nigeria, ambaye hakuwa na imani ya kutibiwa Zanzibar, lakini kutokana na uwezo uliopo wa kitengo hicho mgonjwa huyo alitibiwa na hatimaye baada ya kupona, alianza kuipa sifa Zanzibar na kutoa taarifa katika mitandao ya kijamii.

Dk. Mwinyi alisema kuna haja ya kuwapongeza madaktari wazalendo kuanza kutoa huduma hizo za kibingwa ambazo ni ngumu, jambo ambalo wameonesha kwamba inawezekana katika kutekeleza ndoto zake. Alisema aliona ni bora kuonana na madaktari katika kitengo hicho kwa ajili ya kuwapongeza kutokana na kufanya kazi katika mazingira magumu.

Alisema kazi inayofanywa na kitengo hicho ni nzuri kwa sababu imesaidia kupunguza wagonjwa waliokuwa wakisafirishwa nje ya nchi au Tanzania Bara kwa matibabu ya ziada.

"Nimewaita hapa kwa ajili ya kuwapongeza kutokana na kazi kubwa mnayoifanya ya kutoa matibabu ya kibingwa, hivyo kupunguza mzigo wa serikali kusafirisha wagonjwa nje ya nchi," alisema.

Alisema serikali inaendelea na azma yake ya kujenga hospitali ya kisasa huko Binguni Wilaya ya Kati Unguja na kituo cha kutoa elimu ya mafunzo kwa madaktari wengine.

Alisema ujenzi wa kituo hicho kwa kiasi kikubwa utasaidia na kuwawezesha wananchi kupata huduma za afya nchini na kupunguza kusafirisha nje ya nchi.

Aidha, Dk. Mwinyi alimpongeza daktari bingwa, Prof. Jose Piquer Belloch, kwa juhudi zake kwa kushirikiana na madaktari wazalendo katika kazi ya kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Zanzibar.

"Leo nimefurahi sana, nakupongezeni kwa kazi kubwa mnayoifanya ambayo imeipa sifa kubwa Zanzibar katika kutoa huduma za afya za kibingwa," alisema.

Mapema mkuu wa kitengo cha upasuaji wa ubongo, uti wa mgongo na mishipa ya fahamu, Dk. Said Idrissa Ahmada, alisema idara hiyo ilianzishwa katika mwaka 2014.

Aliongeza kabla ya hapo Prof. Jose alimfanyia upasuaji mkubwa mtoto kutoka Makunduchi Mkoa wa Kusini Unguja na kufanikiwa licha ya changamoto nyingi, na hapo ndipo juhudi za kuimarisha kitengo zilipoanza. Alisema tangu kuanza kutoa huduma hizo mwaka 2014, wamefanikiwa kufanya upasuaji, ukiwamo wa vichwa maji, mgongo wazi, uvimbe wa ubongo na mishipa ya fahamu 1,700.

Prof. Bbellochi, raia wa Hispania, kutoka Taasisi ya Maendeleo ya Elimu inayohusiana na upasuaji wa mishipa ya fahamu (NED), alisifu ushirikiano anaoupata katika kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NAFASI ZA SHULE

Keland Nursery and Primary School iliyopo Salasala Rtd inatangaza Nafasi Za Awali Na Msingi. Mawasiliano :0713327613.

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa*

## KUPOTEA KWA CHETI



**BEATRICE MASHASHI SAID** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S5115-0015** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **OLASITI** mwaka **2015,**yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Polisi taarifa AR/RB/5900/2018**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**Kingolwira**
**Usimamizi wa mirathi**
**04/2021**

Ombi la **SALMA SUDI AMIRI** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **KASHINDE BORI NGOMA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 09/4/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 24/02/2021**

## TANGAZO LA KUPOTELEWA KADI YA GARI.

**Deogratias Alphonce Lyamuya** Mkazi wa Wilaya ya Meatu Mkoani Simiyu anatangaza kupoteza kadi yake ya gari aina Nissan **DATSUN** yenye namba za usajili **T923 AMT,**Injini namba **SD 23121019** na cheses namba **AGY 720100679**

Kadi hiyo ilipotea mwaka jana wakati akihama kutoka nyumba moja kwenda nyingine na kutolewa taarifa polisi tarehe **12/2/2021**

Anaomba yoyote atakayekuwa ameiokota aiwasilishe katika kituo cha polisi Wilaya ya Meatu

Taarifa imetolewa kituo cha polisi kwa **RB namba SIM/MEA/RB/106689/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MÀHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NO 131/2020**

**MDAI WINFRIDA SHAYO**
**DHIDI YA**
**MDAIWA JUMA MANGO**

**Ombi la Mdai WINFRIDA SHAYO**
**Madai ya pesa 1,100,000Ths**
Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauril tajwa hapo juu bila kukosa.
Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 10 Mwezi 3 Mwaka 2021 saa 8:30 Asubuhi/ Alasiri.
Angalia Kama hukuhudhuria/hamtohudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha Kama Umepokea/ Mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/m-meshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Màhakama hii leo tarehe 17 Mwezi 2 Mwaka 2021

**HAKIMU**
**MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**MOROGORO**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**NDUGU ALEX GEORGE MINAI** amepotelewa na kadi ya bajaji aina ya **TVS KING** yenye usajili namba **MC 190 AHV, CHASSISS N A M B A MD6M14PK5D4A79690.** KWA YOYOTE ATAKAE ONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. **RB NA.MORO/MORO/RB/108845/2021.**

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**(JUDIACIARY)**
**KATIKA MÀHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**MOROGORO**
**SHAURI LA MIRATHI NA.02/2021**
**SHANGWE MUZE**
**MGHENI................................ MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**DYNESS MUZE MGHENI.........MAREHEMU**

Màhakama hii inakufahamisha kwamba mwombaji amefungua maombi ya kuwa
Msimamizi wa mirathi, nakala ya madai hayo yanapatikana katika mahakama hii.
Shauri limepangwa kutajwa mnamo tarehe 16/03/2021 saa 2:00 asubuhi na kwa
Yeyote anayehusika na mirathi hayo anaombwa kufika katika mahakama ya hakimu
Mkazi Morogoro.

Zingatia kwamba kutofika kwako tarehe hiyo, shauri litaanza kusikilizwa bila ya wewe
Kutaarifiwa tena, na maamuzi kutolewa.

Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Màhakama hii leo tarehe 25 mwezi 02 mwaka 2021

## NAMPULA AUCTION MART
## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

### MAREKEBISHO

February 24, 2021 tulitangaza kwenye Gazeti la Nipashe kwa niaba ya NCBA BANK TANZANIA LIMITED Majina ya Wadaiwa na maelezo ya Dhamana lakini maelezo mengine yalikatika hayakutoka.

Maelezo hayo ni kama ifuatavyo:

**MDAIWA:** Geoffoson INVESTMENT LTD
**DHAMANA:** Nyumba
**MAELEZO YA DHAMANA:** Plot no 434 bock "b" ct no 86418 Kinyerezi Wilaya ya Ilala, I.NO Geoffoson GAEOFREY KAHWILI
**TAREHE YA MNADA:** 20/03/2021

**MDAIWA:** Geoffoson INVESTMENT LTD
**DHAMANA:** Nyumba
**MAELEZO YA DHAMANA:** Plot no 616 bock "s" ct no 36359 mbulu area, Kahama I.NO GEOFREY MALIYAWONDA
**TAREHE YA MNADA:** 17/03/2021

**MDAIWA:** LUSEKELO JOSEPH KASSANGA
**DHAMANA:** Nyumba
**MAELEZO YA DHAMANA:** Plot no 1 bock "f" ct no 125899 Malamba Mawili Wilaya ya Ubungo, I.NO LUSEKELO JOSEPH KASSANGA
**TAREHE YA MNADA: 20/03/2021**

Masharti mengine yanabakia kama yalivyo kwenye tangazo lililotoka.

**Uza,**

**Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**

**Tupigie 0782253676**




OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Nyumba 500 ziliteketezwa Tigray

**Gijet,** ETHIOPIA

ZAIDI ya nyumba 500, ziliteketezwa kwa makusudi katika mji wa Gijet, jimboni Tigray nchini Ethiopia.

Utafiti wa Shirika la Satellite Imagery, umebainisha, na kwamba bado kuna mzozo unaoendelea jimboni humo.

Waziri Mkuu, Abiy Ahmed, alitangaza Novemba mwaka jana kuwa, wanajeshi wake walifanikiwa kudhibiti wanajeshi wa Tigray People's Liberation Front (TPLF), waliokuwa watiifu wa serikali ya Tigray.

**Kadhalika, wanasiasa wa ngazi za juu duniani walisema mabadiliko ya tabianchi ni kitisho kikubwa cha amani.**

Hata hivyo, ilibainika kuwa bado kuna vita vinavyoendelea kwa baadhi ya sehemu za jimbo hilo, kwa mujibu wa wenyeji na Umoja wa Mataifa.

Serikali ya Ethiopia ilikiri kuwapo kwa visa vichache vya ufyatulianaji risasi Jimbo la Tigray, ila hali ya usalama jimboni humo imedhibitiwa.

Kaimu Kiongozi wa Serikali, jimboni Tigray, Mulu Nega, alisema ameetuma kamati maalamu kuchunguza hali hiyo katika mji wa Gijet.

Ripoti ya Shirika la Utafiti wa mikasa la DX Open Network, lenye makao yake nchini Uingereza ilisema picha ilizodadisi za moto katika mji wa Gijet, moto huo haukuwa ajali.

DX Open Network hata hivyo katika ripoti yake haijaeleza ni nani waliohusika katika mkasa huo wa moto.

Serikali ya Ethiopia na ile ya Tigray, zimekataa kuhusishwa na mzozo wa Jimbo la Tigray, wakati serikali bado inadhibiti mawasiliano jimboni humo. **RFI**

## Waziri Mkuu Armenia atakiwa kujiuzulu

**Yerevan,** ARMENIA

WAZIRI Mkuu wa Armenia, Nikol Pashinyan, amemfuta kazi mkuu wa utumishi jeshini, akimtuhumu kwa kutaka kumpindua jana.

Awali, mkuu huyo wa jeshi alikuwa amemtolea wito Pashinyan kujiuzulu kwa hiari yake, kuitikia wito wa waandamanaji wanaomkosoa kwa namna serikali yake ilivyoushughulikia mgogoro baina ya nchi hiyo na Azerbaijan juu ya jimbo la Nagorno-Karabakh.

Waziri mkuu huyo alitumia mtandao wa Facebook kuwataka wafuasi wake kujitokeza kwa wingi mitaani kumuunga mkono alichosema ni jaribio la mapinduzi ya kijeshi dhidi yake.

Hadi sasa, haijafahamika endapo jeshi limedhamiria kutumia nguvu kumwondoa madarakani endapo hakukubali ushauri waliompa wa kuondoka mwenyewe. **DW**

## Marekani kutoa ripoti mauaji ya Jamal Khashoggi

**Washington,** MAREKANI

MAREKANI inajiandaa kuchapisha ripoti kuhusu mauaji ya mwandishi wa habari wa Saudi Arabia, Jamal Khashoggi.

Vilevile, Ikulu ya White House ilisema kuwa Rais wa Marekani Joe Biden anapanga kuzungumza hivi karibuni na Mfalme Salman wa Saudi Arabia. Khashoggi aliuawa mwaka 2018 katika ubalozi wa Saudia jijini Instanbul, Uturuki.

Biden alisema alitaka kutathmini upya uhusiano wa nchi yake na Saudi Arabia, akisema kuwa Marekani angependa kuwa na mazungumzo moja kwa moja na Mfalme Salman.

Rais aliyeondoka madarakani, Donald Trump awali alikuwa akituhumiwa kuzibia masikio madai ya ukiukaji wa haki za binadamu unaohusishwa na mrithi wa Saudi Arabia, Mohammed bin Salman, lakini maswali yanabaki juu ya msimamo wa Rais wa Marekani Joe Biden. **BBC**



Wanajeshi wakikabiliana na waandamanaji wanaounga mkono demokrasia, wakati jeshi lilipokuwa likitoa msaada huko Yangon, nchini Myanmar, jana. **PICHA: REUTERS**

## Bobi Wine ahojiwa umiliki gari kifahari

**Kampala,** UGANDA

MAMLAKA nchini Uganda, zinamtaka kiongozi wa Chama cha National Unity Platform (NUP), Robert Kyagulanyi (pichani) kuweka wazi jinsi alivyopata gari lake jipya la kifahari kufikia Machi 31.



Katika mkutano na waandishi wa habari mjini Kampala, Mkaguzi Mkuu wa Serikali, alitangaza kuwa viongozi wote nchini humo, wataanza kutangaza mali zao, vyanzo vyake na madeni waliyonayo kwanzia Machi Mosi, mwaka huu.

Akijibu maswali kutoka kwa waandishi wa habari, Mkurugenzi wa Kanuni ya Maadili katika Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Annet Twine, alithibitisha kwamba viongozi watahitajika kutangaza mali zao, zawadi na misaada waliyopokea katika juhudi za kukabiliana na ufisadi.

Wiki iliyopita Kyagulanyi maarufu Bobi Wine, mgombea wa urais wa zamani, alizindua gari lake jipya aina ya SUV na Cruiser V8 lenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni moja za Uganda, ambalo alidai haliingii risasi. **BBC**

## 36 wauawa kwa saa 48 Nigeria

**Katsina,** NIGERIA

WATU 36 wameuawa baada ya kushambuliwa na watu wenye silaha.

Mashambulizi mawili yaliyofanyika Kaskazini mwa Nigeria, yasisababisha vifo hivyo, kulingana na maofisa na ndugu wa waathiriwa.

Pia taarifa zinasema, mashambulizi hayo yalifanyika katika muda wa saa 48 zilizopita jana, katika majimbo ya Kaduna na Katsina.

Aidha, washambuliaji hao hawakujulikana pia walisababisha watu kadhaa kujeruhiwa.

Kadhalika, washambuliaji walichoma moto nyumba kadhaa na kusababisha watu kuhama makazi yao.

Wiki iliyopita, watu wenye silaha wasiojulikana walishambulia shule ya sekondari katika Jimbo la Niger, nchini Nigeria na kuwateka nyara wanafunzi 27, wafanyakazi pamoja na familia zao. **RFI**



# GUARDIOLA ATAMBIA FEDHA ZA MAN CITY

**BUDAPEST,** Hungary

MANCHESTER City imefanikiwa kuweka rekodi ya kushinda mechi 19 mfululizo kwa sababu ya fedha nyingi walizotumia kununua "wachezaji wa ajabu", ametania Pep Guardiola.

Ushindi wa City wa mabao 2-0 dhidi ya Borussia Monchengladbach mjini Budapest kwenye mchezo kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16, imewaweka vinara hao wa Ligi Kuu England kwenye nafasi nzuri ya kufuzu hatua ya robo fainali.

Guardiola aliwaingiza Sergio Aguero, Ferran Torres na Riyad Mahrez kutokea benchi pale kwenye dimba la Puskas, huku John Stones, Kevin De Bruyne na Benjamin Mendy walikuwa miongoni mwa wachezaji ambao hawakutumika.

Bernardo Silva na Gabriel Jesus kila mmoja alifunga bao moja, wakiendeleza ushindi tangu Desemba 16, mwaka jana.

Wakati alipoulizwa kuhusu sababu ya kikosi chake kuwa na mafanikio, Guardiola alionekana kama anajivunia fedha.

"Tuna fedha nyingi za kununua wachezaji wa ajabu," alitania.

"Muda wote tunashinda kwa fedha, huu ni ukweli. Na bila ya wachezaji wazuri wenye ubora, hatuwezi kufanya hivyo.

"Katika kundi hili kuna wachezaji bora na wanauhusiano mzuri wa kucheza pamoja na kushinda mchezo."

# Zidane: Hatukucheza vizuri dhidi ya Atalanta

**BERGAMO,** Italia

ZINEDINE Zidane amekubali majeruhi yameiathiri Real Madrid, lakini hakuridhika na kiwango walichocheza wakati wakiibuka na ushindi dhidi ya Atalanta iliyokuwa na wacheaji 10 kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kiungo wa Atalanta, Remo Freuler alitolewa kwa kadi nyekundu baada ya kumfanyia faulo, Ferland Mendy dakika ya 17 kwenye mchezo huo wa kwanza wa hatua ya 16 uliochezwa kwenye Uwanja wa Gewiss, Jumatano.

Licha ya Madrid kutawala mchezo, lakini walipiga mashuti matatu tu yaliyolenga bao hadi Mendy alipofunga bao lake la kwanza zikiwa zimebakia dakika nne mpira kumalizika.

Los Blancos hao ambao walikuwa na wachezaji kama Karim Benzema na Eden Hazard ambao walirudi kutoka majeruhi, walikosa mbinu za kupenya ngome ya Atalanta hadi Mendy alipofunga bao hilo.

Zidane anajua ushindi huo wa tano mfululizo kwa Madrid haukuwa katika kiwango kizuri, lakini aliahidi kurekebisha makosa kwenye mchezo wa marudiano utakaopigwa Machi 16, mwaka huu.

Kocha huyo wa Madrid alisema: "Hatukucheza vizuri, lakini jambo la muhimu ni matokeo.

"Mwishoni tulifunga, kufunga lilikuwa jambo la muhimu sana kwetu. Bado tunatakiwa kucheza mchezo wa pili, lakini ni matokeo mazuri."





# *Joshua amtaka Tyson ulingoni*

**LOS ANGELS,** Marekani

BONDIA Anthony Joshua amemwambia, Tyson Fury kama anataka kupigana na yeye anafahamu wapi kwa kumpata.

Joshua na Tyson wanaweza kupanda ulingoni mara mbili mwaka huu, huku pambano la kwanza likitarajiwa kuwapo Juni, na bingwa huyo wa mikanda ya WBO, WBA Super na IBF tayari amethibitisha wapo kwenye hatua za mwisho kukamilisha mipango yao.

Akizungumza na Sky News, Joshua alibainisha kuwa wanatazama tarehe nzuri ya pambano lao litakalochezwa ifikapo Juni.

Mabondia hawa wamekuwa wakitupiana maneno, na bila shaka kila mmoja anasubiri kwa hamu kuthibitisha kuwa yeye ndiye mfalme.

Joshua amesema kuwa yeye yupo tayari, na Tyson anaelewa wapi kwa kumfuata na kukutana naye.

"Niko tayari na ninasubiri kwa hamu sana hili pambano, ninachotaka ni kupigana, kupigana, kupigana! Nasubiri kwa hamu sana kurejea ulingoni," alisema Joshua.

# Van Dijk, Jota warejesha matumaini Liverpool

**LIVERPOOL,** England

DIOGO Jota anakaribia kurudi dimbani kwa Liverpool, huku mwenzake Virgil van Dijk pia akionyesha ishara nzuri ya kuendelea kupona.

Jota hajaichezea Liverpool tangu Desemba, mwaka jana baada ya kuumia goti.

Nyota huyo wa kimataifa wa Ureno, alianza maisha vizuri pale kwenye dimba la Anfield, ambapo alifunga mabao tisa katika mechi 17 alizocheza baada ya kujiunga akitokea Wolves, Septemba, mwaka jana.

Jota, juzi Jumatano alifanya mazoezi dakika zote na kikosi cha kwanza cha Jurgen Klopp pale kwenye kituo chao cha AXA.

Kukosekana kwa Van Dijk ambaye aliumia goti kwenye mchezo wa Everton baada ya kugongana na golikipa, Jordan Pickford Oktoba, mwaka jana pale katika dimba la Goodison Park, kumeifanya safu ya ulinzi ya Liverpool kuyumba.

Pia kuumia kwa Joe Gomez na Joel Matip kuliiteteresha kabisa safu hiyo ya ulinzi kwa kikosi hicho cha Klopp msimu huu, huku Jordan Henderson naye akiumia.

Tofauti na Jota, kurudi kwa Van Dijk hakutarajiwi kuwa hivi karibuni, lakini ameanza mazoezi ya peke yake.

Liverpool imeshinda mechi nne na kutoka sare tatu kati ya nane wakiwa na Van Dijk msimu huu, ikiwamo waliyopokea kichapo cha mabao 7-2 kutoka kwa Aston Villa.







# LEWANDOWSKI AINGIA REKODI YA MABAO UEFA

**ROME,** Italia

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Robert Lewandowski ameendeleza kuweka rekodi katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, baada ya kuisaidia timu yake kuibuka na ushindi wa 4-1 dhidi ya Lazio.

Lewandowski sasa amefunga jumla ya mabao 72 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa ni mchezaji wa tatu katika orodha ya wachezaji waliofunga mabao mengi kwenye historia ya michuano hiyo.

Mshambuliaji huyo ameingia katika orodha ya wachezaji waliofunga mabao mengi kwenye mashindano hayo akishika nafasi ya tatu nyuma ya Cristiano Ronaldo na Lionel Messi.

Ronaldo hadi sasa amefunga jumla ya mabao 134, huku Messi akifunga magoli 118 na nafasi ya nne yupo Raul aliyefunga mabao 71.

Pia Lewandowski amekuwa mchezaji wa kwanza katika wachezaji walifunga mabao mengi ya Ligi ya Mabingwa tangu kuanza kwa msimu uliopita, akiwa na mabao 19.

Anafuatiwa na Erling Haaland mwenye mabao 18, Kylian Mbappe mabao 10, Karim Benzema (9), Serge Gnabry (9), Alvaro Morata (9) na Neymar (9).

# *Aarons agonganisha klabu kubwa Ulaya*

**LONDON,** England

LICHA ya kuwa anacheza kwenye Ligi Daraja la Kwanza nchini England katika Klabu ya Norwich City, mlinzi, Max Aarons amezifanya klabu kubwa barani Ulaya kukimbizana kuwania saini yake.

Aarons mwenye umri wa miaka 21 anatajwa kama mchezaji mwenye nyota njema akiwa kama beki hodari wa pembeni.

Klabu za Manchester United, Barcelona, Bayern Munich na AS Roma zimehusishwa na Aarons katika vipindi tofauti tofauti.

Imeripotiwa kuwa, Everton nao wameingia kwenye kinyang'anyiro cha kumsaka Aarons ambaye wanamtizama kama mrithi sahihi wa nahodha wao, Seamus Coleman.

Ifikapo Julai, 2021 Coleman atakuwa amebakiza mwaka mmoja tu katika mkataba wake na Everton.

Licha ya kuwa Norwich City haichezi Ligi Kuu England, klabu hiyo haitopokea dau lolote la chini ya pauni milioni 30 hadi 35 kama sehemu ya usajili wa Aarons.



# DO… ZA SOKA
## MA… A ULAYA




# HAALAND AWEKWA RASMI SOKONI EPL

## Wakala wake ametamba hakuna kocha ambaye hataki kufanya kazi na mshambuliaji...

**LONDON,** England

MINO Raiola ambaye ni wakala wa nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland ameanza mbwembwe za mteja wake huyo, huku akipelekea vuguvugu la mchezaji huyo kuondoka klabuni hapo katika majira ya joto yajayo.

**Akizungumza na vyombo vya habari, Raiola alianza kwa kumnadi Haaland akidai hakuna kocha yoyote duniani asiyependa kufanya kazi na mshambuliaji huyo.**

"Kuna timu 10 tu duniani ambazo zina uwezo wa kiuchumi wa kumnunua Erling Braut Haaland. Na nne kati ya hizo 10 zipo Ligi Kuu England," alisema akinukuliwa na vyombo vya habari vya Uingereza.

"Sidhani kama kocha au mkurugenzi wa michezo wa klabu yoyote duniani atasema hapana hamuhitaji Haaland."

Haaland amefunga mabao 10 katika mechi saba alizoitumikia Borussia Dortmund kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Hiyo imemfanya kuwa mchezaji wa pili kati ya wachezaji waliofunga mabao mengi kwenye mashindano hayo msimu huu, akitanguliwa na Robert Lewandowski mwenye mabao 19.

Nyota mkongwe wa Ujerumani, Lothar Matthaus amemtaka mshambuliaji huyo wa Timu ya Taifa ya Norway kuondoka Borussia Dortmund kama anahitaji kuendeleza kipaji chake.

Haaland ambaye ana umri wa miaka 20, alijiunga na vigogo hao wa Ujerumani katika dirisha dogo la Januari mwaka huu.

Real Madrid, Barcelona, Manchester United, Manchester City na Chelsea zote zimeonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji huyo ambaye ada yake ya uhamisho iliyoko kwenye mkataba ni Euro milioni 75, lakini kifungo hicho kitaanza kufanya kazi mwakani.

## ZISIKUPITE

### CITY KUSAJILI MAJEMBE

MANCHESTER City inafikiria kutoa zaidi ya pauni milioni 100 kununua nyota wapya akiwamo mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 20, na kiungo wa kati wa Marekani, Giovanni Reyna mwenye miaka 18, wakati wa dirisha la usajili kipindi cha majira ya joto. ***(90min)***

### ABRAHAM NJIA MOJA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na England, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, hayuko tayari kuingia mkataba mpya, huku klabu hiyo ikiendelea kuhusishwa na Erling Haaland. ***(Metro)***

### SOLKAJAER VS HAALAND

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer amekiri amekuwa akiwasiliana na Erling Haaland mwenye mri wa miaka 20, ambaye alikuwa akimfundisha wakati akiwa mkufunzi wa Klabu ya Molde. ***(Sky Sports)***

### UNITED YAIGOMEA SEVILLA

MANCHESTER United haiko tayari kulipa dau la pauni milioni 68 ili kumnunua mlinzi wa kati wa Sevilla na Ufaransa mwenye umri wa miaka 22, Jules Kounde. ***(Mail)***

### LINGARD NYOTA YANG'ARA

WEST Ham itakabiliana na ushindani dhidi ya Leicester City kama itataka kumsajili moja kwa moja kiungo wa kati wa Manchester United, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28. ***(Express)***

### HENDERSON SOKONI

MANCHESTER United imeweka wazi thamani ya golikipa wake, Dean Henderson ni pauni milioni 40, kama wakiamua kumuuza. ***(Express)***

### NORWICH KUTAJIRIKA

KLABU ya Norwich City inatarajia itapokea kiasi cha pauni milioni 35 kwa kumuuza mlinzi wa England, Max Aarons mwenye umri wa miaka 21, ambaye analengwa na Manchester United. ***(Metro)***

### AARONS AGEUKA LULU

EVERTON haijawasiliana na Norwich kuhusu mkataba wa Max Aarons na inatarajia ushindani mkali kutoka kwa Manchester United, Bayern Munich na Barcelona. ***(Mail)***

### VAN AANHOLT KUSEPA

MLINZI wa Crystal Palace na Uholanzi, Patrick van Aanholt, 30, ameanza mazungumzo na klabu ambayo haijatajwa iliyofuzu katika Ligi ya Mabingwa Ulaya. Mkataba wa mchezaji huyo unakamilika mwisho wa msimu huu. ***(Football Insider)***

### MATA SAFARI IMEIVA

MANCHESTER United haitatumia kifungu cha kuongeza mkataba wa mwaka mmoja zaidi kwa kiungo wake wa kati, Juan Mata mwenye umri wa miaka 32. ***(MEN)***

HABARI MICHEZO

# SIMBA MGUU SAWA KUMUUZA MIQUISSONE

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema milango iko wazi na wako tayari kukaa meza moja na klabu yoyote kutoka nje ya Tanzania inayohitaji kumnunua mchezaji aliye katika kikosi chake ambacho sasa kinashiriki hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

**Kauli hiyo imekuja baada ya wachezaji wa Simba kuonyesha kiwango kizuri ikiwamo, Luis Miquissone na kuvutiwa na baadhi ya mawakala na klabu mbalimbali zilizoshuhudia mchezo wa Kundi A kati ya Simba dhidi ya Al Ahly, ambao ulimalizika kwa wenyeji kushinda bao 1-0.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema hawatakuwa 'wajinga' kuacha hela endapo klabu yoyote duniani itakuja na dau kubwa kwa ajili ya kumnunua Miquissone.

Manara alisema wanatambua kwa sasa kuna timu nyingi duniani ambazo zinahitaji saini ya nyota huyo kulingana na uwezo wake anaonyesha katika kila mechi.

"Tutakuwa wajinga kuacha hela endapo timu ikija na dau zuri, litakuwa na maslahi mazuri kwa Simba na mchezaji ukizingatia maisha ya mchezaji yoyote ni kucheza vizuri na kujiuza ili kupata fedha.

"Sasa ipo wazi duniani kote kuna mawakala walikuwapo Uwanja wa Mkapa na wale ambao wanafuatilia mpira, Miquissone nina imani kwa sasa yupo sokoni na anahitajika hapa Afrika hata nje ya mipaka hii," alisema Manara.

Alisema ikitokea timu ikihitaji saini ya nyota huyo lazima timu ijipange kupata huduma yake kwa sababu ni mchezaji ghali kwa sasa.

"Kwa uongozi wa Simba kwa sasa umekuwa makini sana katika suala la kuwekeza soka la vijana ila kupata mazalio mapya, lakini kuhakikisha kutafuta mawakala ambao hata wakituletea wachezaji ambao watakuja kuziba nafasi ya watakaopata bahati ya kuuzwa," Manara alisema.

Kuhusu kufanya vizuri kwa Simba, alisema siri kubwa ni umoja na mshikamano wa wanasimba wote na ana imani wakiendelea hivyo wataendelea kupata matokeo mazuri na kusonga mbele kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Mafanikio yote ambayo unayoona na kufanya vizuri kwa Simba ni umoja na mshikamano wetu, ukiona tunafanya vibaya ujue kuna chokochoko na figisu figisu, hivyo lazima tucheze na kauli mbiu za wazee wetu," alisema Manara.

Alitaja malengo ya timu yao msimu huu yako matatu ambayo ni kutwaa ubingwa wa ligi, Kombe la FA na lengo mama ni kuvuka katika hatua ya makundi ya michuano ya kimataifa.

"Nafasi ya Simba kufuzu ipo ni kupambana kwenda kutafuta pointi muhimu kwenye mechi zetu mbili ikiwamo dhidi ya Al Merrekh, ambayo tunaenda kucheza Khartoum, Sudan," alisema Manara.

Aliongeza baada ya kumaliza mechi dhidi ya Al Ahly, viongozi walikutana na benchi la ufundi ili kuwahimiza kuendelea kupambana kupata matokeo mazuri katika mchezo unaofuata wa Kombe la FA dhidi ya African Lyon.

"Simba tumekuwa na shida ambayo sielewi tunapotoka kucheza mechi kubwa na tunapokwenda kucheza mechi ndogo huwa hatufanyi vizuri, nimemsisitiza Matola (Selemani), asichukulie poa mechi dhidi ya African Lyon hapo kesho (leo)."

"Bora kufungwa na Al Ahly na afadhali kuotolewa katika hatua ya makundi na sio kufungwa na African Lyon, hivyo msimu huu ubingwa wa ligi na FA ni lazima, tunaenda kupambana kufikia malengo," alisema Manara.



Viongozi wa Timu za Huduma FC, Mabomba na Temeke Squad wakionyesha seti za jezi walizokabidhiwa na Chama cha Soka cha Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), kwa ajili ya kwenda kushiriki Ligi ya Mabingwa wa Mikoa itakayofanyika kwenye vituo mbalimbali kuanzia Machi 4, mwaka huu. Kushoto ni Mweka Hazina wa DRFA, Issa Masoud na mwenyekiti wa chama hicho, Lameck Nyambaya. **PICHA: DRFA**

## Mastraika JKU wamliza kocha

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa JKU, Omar Khamis "Matu" amewaangushia lawama washambuliaji wake kwa kushindwa kupachika mabao katika mchezo wa kwanza wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Zanzibar uliochezwa juzi Visiwani hapa.

JKU ilibanwa mbavu na Kipanga na kumaliza dakika 90 kwa sare ya bila kufunga kwenye Uwanja wa Mau A.

Matu aliliambia gazeti hili baada ya kumalizika mchezo huo timu yake haikucheza vizuri ikilinganishwa na alivyotegemea.

Kocha huyo alisema wachezaji wake walitengeneza nafasi nyingi za wazi za kufunga, lakini kukosa umakini kwa washambuliaji wake walijikuta mipira yote ikitoka nje na kushindwa kupata mabao.

"Mchezo ulikuwa mgumu, lakini timu yangu haikucheza vizuri sana, mabeki na washambuliaji walikuwa kama mawazo yao hayapo uwanjani, tumepoteza nafasi nyingi sana za wazi," alisema Matu.

Hata hivyo alisema kwa sasa wanajipanga kuyafanyia kazi makosa aliyoyabaini ili yasijirudie tena kwa ajili ya kuelekea mechi yao inayofuata dhidi ya KMKM.

Naye Kocha Mkuu wa Kipanga, Rashid Lato, alisema kutoka sare katika mchezo huo dhidi ya JKU ni kawaida kwa sababu timu zote huanza kwa presha katika mechi za mzunguko wa pili kwa sababu ya kuwinda pointi tatu muhimu.

Ligi Kuu Zanzibar itaendelea tena leo kwa Malindi kumenyana na Chuoni kwenye Uwanja wa Amaan wakati katika Uwanja wa Mao A, Polisi watawakaribisha Mafunzo.



## Mgosi kuondoka Simba Queens

**Na Saada Akida**

BAADA ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 kwenye uwanja wa nyumbani dhidi ya Ruvuma Queens, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Mussa Hassan 'Mgosi' amesema matokeo ya mchezo huo hayajamwondoa katika mbio za kutetea ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania wanaoushikilia.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mgosi alisema ana imani na kikosi chake kitapata matokeo mazuri katika mechi zijazo licha ya kupunguzwa kasi na kikosi hicho cha Ruvuma Queens.

Mgosi alisema kwa sasa anaendelea kufanyia kazi upungufu uliyojitokeza katika mchezo huo uliopita ili kuendelea kutafuta pointi tatu muhimu katika mechi ijayo ya ugenini dhidi ya JKT Queens.

"Bado hatujakata tamaa katika mbio za kutetea ubingwa wetu, tunafanyia kazi makosa yetu ili kuboresha sehemu zote na kuwa imara, nina imani msimu huu tuna uwezo wa kutetea ubingwa huo, tukikosa basi nitaacha ngazi kufundisha Simba Queens," alisema Mgosi.

Aliongeza ligi hiyo imekuwa na ushindani mkubwa, lakini hana hofu juu ya kasi ya wapinzani wao Yanga Princess, ambayo inaongoza ligi hiyo na kupata matokeo ya kuvuna pointi tatu kila mechi.

"Kwa sasa ni ngumu kubashiri ubingwa wa msimu huu unaenda timu gani, kwa imani yangu kwamba mwishoni mwa msimu huu hasa baada ya sisi tutakapocheza dhidi ya Yanga ndio bingwa atajulikana," alisema Mgosi.

# Michezo

Ijumaa Februari 26, 2021

Nipashe




Haaland awekwa rasmi sokoni Ulaya UKURASA 22



Mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus (kushoto), akifunga bao la pili kwa timu yake huku golikipa wa Borussia Mönchengladbach, Yann Sommer (kulia), akishindwa kuokoa hatari hiyo katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa jijini Budapest, Hungary juzi usiku. City ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAITISHA AFRICAN LYON

## ●●● Yatamba inahitaji kushinda ili kukamilisha...

**Na Somoe Ng'itu**

HATUTAWADHARAU! Hayo ni maneno ya mabingwa watetezi, Simba kuelekea mchezo wa mzunguko wanne wa mashindano ya Kombe la FA dhidi ya African Lyon utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

**Simba ndio mabingwa watetezi wa mashindano hayo yanayochezwa kwa mfumo wa mtoano na bingwa wake hupata tiketi ya kushiriki michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.**

Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes aliliambia gazeti hili jana, kikosi chake kimejipanga kuhakikisha kinapata ushindi mapema na kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo.

Gomes alisema mechi zote ambazo timu yake inacheza ni sawa na fainali kwa sababu wanahitaji kukamilisha malengo waliyonayo ya kuchukua mataji.

Mfaransa huyo alisema katika soka hakuna mechi ndogo wala kubwa kwa sababu kila timu hujiandaa kupata matokeo chanya na amejiandaa kukabiliana na ushindani wowote kwenye mchezo huo.

"Kila siku tunakutana na changamoto tofauti, tumesahau matokeo ya mechi iliyopita na sasa akili yetu ni mchezo wa Kombe la FA, tunatarajia kukutana na ushindani hasa kwa sababu ni mashindano ya mtoano, tumejipanga kuendeleza kasi yetu tuliyonayo kwa sababu tunahitaji ubingwa wa michuano hii pia," Gomes alisema.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema wataingia katika mchezo huo kwa 'nguvu kubwa' kuhakikisha wanapata ushindi.

"Tumekuwa na tabia ya kupoteza mechi ndogo baada ya kumaliza mchezo dhidi ya timu kubwa, nimeongea na Matola (Selemani- Kocha Msaidizi) kwa ajili ya kuongeza msisitizo, mimi kwangu ni bora kufungwa 2-0 na Al Ahly, lakini sio African Lyon, tutaingia kwa nguvu ile ile tuliyoishia nayo," Manara alisema.

Aliongeza msimu huu Simba imejipanga kufanya vizuri katika Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini lengo kuu ni kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Bara na Kombe la FA.

Naye Mmiliki wa African Lyon inayoshiriki Ligi Daraja la Kwanza, Rahim Zamunda alisema kikosi chake kiko imara na kinaamini kitapata matokeo chanya dhidi ya mabingwa hao watetezi wa michuano hiyo.

"Hatuiogopi wala kuihofia Simba, sisi tuko imara na tayari kwa mchezo wa kesho, tunauwezo ndani na nje ya uwanja, walipo wao tulishapita zamani," Zamunda alitamba.

Tayari Kagera Sugar ya Bukoba iliyowafunga Eagle Stars na wenyeji wa Mlandizi mkoani Pwani, Ruvu Shooting walipata ushindi dhidi ya Mbao zimeshasonga mbele katika hatua inayofuata ya mashindano hayo.

Mechi nyingine za michuano hiyo zinazotarajiwa kuchezwa leo ni kati ya Arusha FC dhidi ya Mashujaa wakati Mtibwa Sugar itawakaribisha JKT Tanzania, huku Yanga ikiwaalika Kengold FC kutoka jijini Mbeya kwenye Uwanja wa Uhuru.

# Namungo rasmi yatinga makundi

**Na Saada Akida**

WAWAKILISHI wa Tanzania katika mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho, Namungo FC wametinga hatua ya makundi licha ya kufungwa mabao 3-1 na wageni CD Primiero de Agosto ya Angola katika mechi ya marudiano iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam jana.

Namungo imesonga mbele kwa jumla ya mabao 7-5, baada ya kupata ushindi wa mnono wa magoli 6-2 katika mechi ya kwanza iliyofanyika Jumapili iliyopita kwenye uwanja huo.

Namungo ilikuwa ya kwanza kupata bao kupitia kwa Sixtus Isabilo dakika ya sita wakati Brian Moyo aliisawazishia De Agosto kwa penalti dakika ya 27 na dakika 51 akafunga goli la pili huku Natael Masuekama akipachika la tatu dakika za lala salama.

Katika hatua hiyo ya makundi, Namungo inayoshiriki michuano ya kimataifa kwa mara ya kwanza iko Kundi D pamoja na timu za Raja Casablaca ya Morocco, Pyraminds (Misri) na Nkana FC ya Zambia.

Namungo ilipata tiketi ya kushiriki mashindano hayo baada ya kumaliza katika nafasi ya pili kwenye michuano ya Kombe la FA msimu uliopita, ikifungwa mabao 2-1 na Simba katika mchezo wa fainali.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042